

**ZUCHU HAKAMATIKI**

Urembo, kazi zake moto Afrika

UKURASA 20



**Coutinho** nje ya dimba hadi Aprili


UKURASA 21

**MAISHA** JANUARI 3, 2021 Nipashe — Baba, Mama na Mwana — *Jumapili*



Ukurasa 10

**Usimwambie mtoto 'usinijibishe', msikilize**



Ukurasa 15

**MAISHA NI NYUMBA**
Dondoo za kukipamba chumba cha kulala



**HARUSI**

Ukurasa 12



**NYWELE ZAKO TU**
**Ukiziachia utapendeza**

Ukurasa 14


# Nipashe JUMAPILI

MWANGA WA JAMII

Jumapili Januari 3, 2021 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • No. 0580449

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US


UKURASA 9

## RIPOTI MAALUM

# NI MAJANGA

• **Wanafunzi** shule binafsi wakaa darasani saa 14 alfajiri hadi giza, Waziri Ndalichako awaka... *Endelea ukurasa 4 & 5*



Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, akimkabidhi hati ya kiapo Katibu wa Baraza la Mapinduzi ambaye ni Katibu Mkuu Kiongozi, Mhandisi Zena Ahmed Said, baada ya kuisaini, hafla iliyofanyika Ikulu Zanzibar jana. **PICHA: IKULU**

## Katibu Mkuu Kiongozi aona fursa za ajira

UKURASA 2

## ACT - Wazalendo yatoa kauli Membe kuondoka

UK. 2




Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu


**MICHEZO** **SIMBA YAANDAA RAMANI YA 'VITA'** UK.24

**MAONI, KATUNI** UK.6

## HABARI KITAIFA

# ACT yatoa kauli Membe kujivua uanachama

**Na Enock Charles**

ALIYEKUWA mgombea urais kupitia Chama cha ACT-Wazalendo, Bernard Membe, amejivua uanachama wake na nafasi yake ya mshauri mkuu wa chama hicho, ikiwa ni takribani siku 170 tangu ajiunge nacho Julai 16, mwaka jana.

Waziri huyo wa zamani wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, alitangaza uamuzi huo juzi usiku, akibainisha kuwa kwa sasa, atakuwa mshauri wa masuala mbalimbali yanayoihusu nchi na kupigania demokrasia ya kweli.

Akizungumzia uamuzi huo wa Membe, Katibu Mkuu wa ACT-Wazalendo, Ado Shaibu, aliiambia Nipashe jana kuwa chama hicho kilikuwa na taarifa za kusudio hilo la Membe kwa muda mrefu na kwamba kinamtakia heri huko aendako.

Shaibu alisema chama hicho hakina kinyongo na uamuzi huo na kamwe hakitajiingiza kwenye malumbano na mwanasiasa huyo, ambaye kabla ya kujiunga nacho, alifukuzwa uanachama ndani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM).

"Taarifa hizi za ndugu Membe kujiuzulu uanachama wa chama chetu na kujivua nafasi zote za uongozi tumezipokea na kimsingi siyo taarifa ngeni kwa sababu tumekuwa tukizifahamu. Ndugu Membe mwenyewe amewasiliana na sisi mara kadhaa. "Hata baada ya Uchaguzi Mkuu, Ndugu Membe ilikuwa ni kana kwamba ameshajiweka pembeni na shughuli za chama.

"Tunachoweza kusema kama chama ni kwamba, sisi ACT-Wazalendo tunao utamaduni wa muda mrefu, mtu yeyote akijiondosha kwenye chama, mara nyingi tunajiepusha na malumbano na tunamtakia kila la heri," Shaibu alisema.

Membe alijiunga na ACT-Wazalendo Julai mwaka jana, baada ya kuvuliwa uanachama wa CCM Februari mwaka jana, akituhumiwa kukiuka maadili ya chama hicho.

Katika hilo, Membe hakuwa mtuhumiwa pekee. Makada wengine waliohusishwa naye ni pamoja na waliowahi kuwa Makatibu Wakuu wa CCM, Yusuph Makamba na Abdulrahman Kinana, ambao walipewa onyo kali na baadaye kusamehewa na vikao vya juu vya chama hicho.



Askari wa usalama barabarani akielekeza abiria katika kituo kikuu kipya cha mabasi kilichogharimu zaidi ya Sh. bilioni 6.8 kilichopo Kijiji cha Tanga, Kata ya Tanga, Manispaa ya Songea, mkoani Ruvuma, ambacho kimezinduliwa mwaka mpya. **PICHA: MICHAEL EMMANUEL**

# Katibu Mkuu Kiongozi mpya aona fursa ajira

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amemwapisha Zena Ahmed Said, kuwa Katibu Mkuu Kiongozi na Katibu wa Baraza la Mapinduzi, huku kiongozi huyo akiahidi kumsaidia Rais kupanua fursa za ajira. Zena aliteuliwa na Dk. Mwinyi kushika nafasi hiyo mwishoni mwa mwaka jana baada ya kustaafu kwa aliyekuwa Katibu Mkuu Kiongozi, Abdulhamid Yahya Mzee.

Hafla hiyo ya kiapo ilifanyika Ikulu mjini Zanzibar jana na kuhudhuriwa na viongozi mbalimbali wa serikali na sekta binafsi.

Akizungumza na waandishi wa habari baada ya kula kiapo, Zena alisema atakuwa mbunifu katika kumsaidia Rais kiutendaji, ili kufikia malengo ya kuwaletea maendeleo wananchi wa Zanzibar.

Alisema kuteuliwa kwake ni neema kubwa kwake, akiahidi atafanya kazi kwa kufuata kanuni, miongozo iliyopo na kuwa mbunifu katika utendaji kazi wake.

"Jinsi maendeleo yatakapopatikana, ninaamini na ajira zitapatikana, hivyo ninamshukuru Rais kwa kuniteua. Wakati unapotenda kazi, ukiwa na hofu ya kuwa mwanamke utashindwa.

"Nafasi yoyote unapopewa, ifanye kwa weledi wa hali ya juu, acha matendo yako na kazi zako zijisemee," alisema Zena ambaye ameweka rekodi ya kuwa Katibu Mkuu Kiongozi wa kwanza mwanamke Zanzibar.

Alisema wanawake wana majukumu mengi, yakiwamo ya familia, hivyo ni vyema kujali kutekeleza majukumu yao kwa wakati stahiki, ili kazi ziendelee vizuri.

"Mimi kofia hii niliyopewa, nikienda katika familia yangu sitoweza kuivaa, bali nitavaa kofia kama ni mama wa familia na kutekeleza majukumu yangu ya familia na nitakapokuwa kazini, nitavaa kofia kwa mujibu wa nafasi yangu," alifafanua.

### WAFURAHIA UTEUZI WAKE

Baadhi ya mawaziri wanawake wa Zanzibar, walisema mwanamke ni jeshi kubwa katika kuleta maendeleo, hivyo wanampongeza Rais kwa kuwapa kipaumbele wanawake kwa kumteua Zena.

Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale, Lema Muhamed Mussa, alisema mwanamke ana nafasi kubwa ya kuleta mabadiliko ya maendeleo kuliko mwanamume.

"Unapomwelimisha mwanamke, umeielimisha jamii nzima, lakini unapomwelimisha mwanamume, unamwelimisha peke yake, hivyo kitendo cha kuteuliwa kwa Zena, kinatupa ari sisi wanawake na kasi ya maendeleo na mabadiliko yatakuwa makubwa," alisifu.

Waziri wa Habari, Vijana na Michezo, Tabia Mwita, alisema uteuzi huo ameupokea kwa furaha na Rais Mwinyi anazidi kujenga imani kwa wananchi kwa sababu anatekeleza yale ambayo aliyaahidi ikiwamo kuwapa nafasi wanawake.

# CHADEMA yatinga rasmi ICC

**Na Enock Charles**

CHAMA cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), kimewasilisha rasmi malalamiko yake katika Mahakama ya Kimataifa ya Uhalifu (ICC) iliyoko Uholanzi, kikidai kutotendewa haki katika Uchaguzi Mkuu wa Oktoba 28 mwaka jana.

Kupitia kwa Makamu Mwenyekiti wake, Tundu Lissu, chama hicho kimelazimika kukimbilia kwenye mahakama hiyo ya kimataifa kikidai kulikuwa na ukiukwaji wa misingi ya uchaguzi wakati wa mchakato wa uchaguzi huo.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Lissu aliyoiita salamu za Mwaka Mpya, tayari chama hicho kimepokea taarifa ya kupokewa kwa malalamiko yao yaliyowasilishwa tangu Desemba 24 mwaka jana.

"Kufuatia kuchafuliwa kwa uchaguzi mkuu na matukio mbalimbali yaliyofanyika kabla, wakati na baada ya Uchaguzi Mkuu wa tarehe 28 Oktoba, chama chetu kilitangaza kitawasilisha malalamiko yake ICC baada ya mawakili wetu kuandaa nyaraka zote zinazohitajika.

"Leo kama sehemu ya salamu zangu za Mwaka Mpya, ninapenda kuwataarifu kwamba tarehe 24 Desemba, Kampuni ya Mawakili ya Amsterdam and Patners wa London, Uingereza na Washington DC, Marekani, iliwasilisha malalamiko kuhusu makosa dhidi ya ubinadamu na dhidi ya CHADEMA kabla, wakati na baada ya Uchaguzi Mkuu," Lissu alisema.

Kwa mujibu wa Lissu, ambaye ni kitaaluma ni mwanasheria, malalamiko hayo huenda yakachukua muda mrefu uchunguzi wake kufanyika, akidokeza kuwa huenda ikawa zaidi ya miaka mitano.

Aliwataka wanachama wa chama hicho kuwa watulivu kusubiri kukamilika kwa mchakato huo wa muda mrefu ambao amedai una matumaini ya kile alichokiita kufufua demokrasia ya kweli.

CHADEMA ilishinda jimbo moja katika Uchaguzi Mkuu huo, huku ikishika nafasi ya pili katika kinyang'anyiro cha kuisaka nafasi ya urais.

HABARI KITAIFA




Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu anayeshughulikia Wenye Ulemavu, Ummy Nderiananga (kushoto), akimsikiliza mmoja wa wawakilishi wa Umoja wa Waendesha Bajaji wenye ulemavu, Juma Bilali (katikati), alipowatembelea kwa lengo la kusikiliza kero zinazowakabili. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Kiwanda chajitosa kutatua tatizo la ajira

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

KIWANDA cha Sukari Kilombero mkoani Morogoro, kimeanzisha mpango maalum wa kutoa nafasi kwa wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) Ndaki ya Kilimo, kushiriki mafunzo ya vitendo sehemu za kazi, ili wapate ujuzi stahiki.

Uongozi wa kiwanda hicho, umesema mpango huo umelenga kuunga mkono jitihada za serikali kukuza ujuzi na kutoa fursa za ajira nchini.

Akizungumzia mpango huo juzi, Meneja Rasilimali Watu wa kiwanda hicho, Beda Chacha, alisema unakwenda sambamba na kutoa ufadhili wa ada na mahitaji yote ya masomo kwa wanafunzi wa vyuo vikuu kwenye masomo ya uhandisi, kilimo na idara zingine za uhasibu na rasilimali watu.

"Tunawapa ufadhili kwa kumlipia gharama za masomo ikiwamo ada na muda wote anapokuwa yupo chuo na baadaye kupewa ajira rasmi," alisema.

Alibainisha kuwa kiwanda kimekuwa na mpango wa kusomesha wanafunzi katika masomo mbalimbali baada ya kubaini dosari ya kukosekana kwa vijana wenye ujuzi wa kufanya kazi viwandani.

Chacha alisema wamebaini vijana wengi wanaohitimu vyuo vikuu, wanakuwa na elimu, lakini hawana ujuzi, huku wakiwa na shauku ya kupewa vyeo vya juu ilhali hawana utaalamu au uzoefu wa kazi wanazotakiwa kuzifanya.

"Kutokana na shida hiyo, kama kiwanda, tukaja na mpango huo wa mafunzo kwa vitendo kwa muda wa miezi mitatu kwa makubaliano lazima afanye kazi kwenye kiwanda chetu," alisema.

Hata hivyo, Chacha alisema idadi kubwa ya vijana wanaojitokeza ni wanaume, huku kundi la vijana wa kike likibaki nyuma, akibainisha kuwa wamebaini jinsi hiyo hawapendi kufanya kazi za viwandani.

"Wanafanya mafunzo ya ndani na nje ya nchi hasa upande wa teknolojia katika viwanda na maeneo mengine ya uzalishaji na usimamizi, lakini kundi la wanawake wanajitokeza wachache, wanaona hizo kazi kama ni ngumu," alisema.

Alisema mpango huo umesaidia vijana wengi waliopo katika idara mbalimbali kwenye kiwanda hicho, wakipitia mafunzo ya vitendo na pia wengine bado wako vyuoni wakiendelea kusoma chini ya ufadhili huo.

Chacha alibainisha kuwa hadi sasa kupitia mpango huo, vijana 53 wamepatiwa ufadhili huo, akiongeza kuwa kiwanda kimeamua kushirikiana na SUA Ndaki ya Kilimo, ili vijana wanaofanya vizuri katika masomo hayo, wapate ufadhili na hatimaye kuhaririwa kwenye kiwanda hicho.

Rasi wa Ndaki ya Kilimo ya SUA, Profesa Bernard Chove, alisema wameingia makubaliano maalum na kiwanda hicho kupeleka wanafunzi, ili kufanya kazi kwa vitendo ikiwa ni sehemu ya utaratibu wa masomo yao.

Profesa Chove alisema mpango huo umeleta manufaa kwa baadhi ya vijana waliofanya vizuri katika masomo yao kutokana na kufanya mafunzo kwa vitendo na kuwa na uhakika wa ajira.

Aliupongeza uongozi wa kiwanda hicho kutoa ufadhili kwa wanafunzi kulingana na mahitaji yao kwa kuwa imeongeza ari kwa wanafunzi kujisomea bila kuwa na hofu ya kukosa ada.

Mmoja wa wanufaika wa mpango huo, Shukuru Thomas, aliyehitimu kozi ya Uhandisi wa Kilimo, alisema alipata ufadhili wa ada mwaka wa nne na kupata mafunzo kwa vitendo kiwandani huko na kisha kuajiriwa akiwa ameandaliwa vizuri.

# Wanafunzi 200 wasoma chumba kimoja

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

WANAFUNZI 218 wa darasa la nne katika Shule ya Msingi Ibadakuli, Manispaa ya Shinyanga, wanasoma katika chumba kimoja kutokana na uhaba wa miundombinu.

Mwalimu Mkuu wa Shule hiyo, Stephen Kudililwa, alibainisha hayo jana wakati Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana na Ajira), Patrobas Katambi, alipozuru katika shule kukagua ujenzi wa vyumba vya madarasa.

Katambi ambaye ni Mbunge wa Shinyanga Mjini, alipatiwa taarifa kwamba shule hiyo kwa sasa ina wanafunzi 1,380, lakini wanafunzi wa darasa la nne wako 218 na wanasoma katika chumba kimoja cha darasa na kusababisha uelewa wao kimasomo kutokuwa wa kuridhisha.

"Mheshimiwa Naibu Waziri, katika shule yetu hii, tunakabiliwa na upungufu mkubwa wa vyumba vya madarasa, kulinganisha na idadi ya wanafunzi waliopo na kusababisha mrundikano wa wanafunzi madarasani hasa darasa la nne ambao wapo 218 kwenye darasa moja.

"Shule hii ina vyumba vinane tu vya madarasa, kuna upungufu wa vyumba 20, na sasa tunajenga vyumba vya madarasa mawili kwa kushirikiana na serikali pamoja na nguvu ya wananchi, ujenzi upo hatua ya kukamilisha boma na umegharimu Sh. milioni tisa," alisema. Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga, Geoffrey Mwangulumbi, alisema halmashauri yake inakabiliwa na upungufu wa vyumba vya madarasa 100 katika shule za msingi 64 na sekondari 34.

Baada ya maelezo hayo, Katambi aliwapongeza wananchi kwa kujitoa kuchangia shughuli za maendeleo, ukiwamo ujenzi wa vyumba vya madarasa, na kuahidi kushirikiana nao kukamilisha ujenzi huo.

# RC autaja urais 2025

**Na Thobias Mwanakatwe**

IKIWA imebaki miaka minne kabla ya kufanyika kwa uchaguzi mkuu mwingine nchini, Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, amesema atashangaa kuona mwaka huu baadhi ya watu wanaanza kujipanga kwa urais wa 2025.

Chalamila ambaye kabla ya kuteuliwa kushika nafasi hiyo, alikuwa Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Iringa, alisema hayo juzi wakati akizungumza na waandishi wa habari kuukaribisha Mwaka Mpya.

"Nitashangaa kama nitaona ni mwaka wa watu kuanza kujipanga na urais wa 2025, nitashangaa kuona ni mwaka wa baadhi ya watu kujipanga kuiba mali za Watanzania," alisema.

Chalamila alisema mwaka 2021 utakuwa ni mwaka wa 'speed' mpya ya utendaji kwa serikali na serikali haitarajii kuona watu wakifanya mambo ya ovyo.

"Ni mwaka ambao tunategemea tusiwaone wezi wa mali za umma, ni mwaka ambao tunategemea tusiwaone wezi wa mali za umma, ni mwaka ambao tunategemea tusiwaone wanafiki na wambea katika taifa," alisema. Aliongeza kuwa mwaka huu wanataka kuona upendo na umoja wa taifa, vyanzo vya mapato na rasilimali za nchi zikiwanufaisha Watanzania na hasa wanyonge.

Alisema ni mwaka ambao wananchi wanataka kuona viongozi wakichapa kazi bila unafiki wakiweka urafiki kando wakitumikia taifa hili kwa uzalendo mkubwa.

"Ni mwaka ambao tunataka kuona hakuna unyanyasaji wa maskini, ni mwaka ambao tunataka tuone kuna matajiri wengi wakiibuka kutokana na utajiri wa Tanzania," alisema.

Chalamila pia alisema serikali itaendelea kuboresha huduma mbalimbali za kijamii zikiwa za afya na kwamba inashangaza watu wengi wanalalamika watu kufa wakati suala la kufa ni la kawaida.

## MAJANGA SHULE BINAFSI

# Darasa la saba na la nne wakaa darasani saa 14, alfajiri hadi giza

- Kisa? Kutafuta ufaulu wapate wanafunzi
- Hakuna wikiendi, bweni & tuisheni lazima
- Agizo la mtaala saa 6, Ndalichako awaka
- Likizo ya corona yaongeza madhila zaidi



Wanafunzi wakiwa katika matukio ya shuleni. Ni sehemu ya umri unaokumbwa na tatizo linalofanana na simulizi ya ripoti hii. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

**Na Christina Mwakangale**

IMEBAINIKA ukiukwaji mkubwa wa kanuni na miongozo ya taaluma kwa baadhi ya shule za binafsi jijini Dar es Salaam, zinazobadilisha utaratibu wa ufundishaji, wenye kuhatarisha kwa kiasi kikubwa afya na usalama wa mwanafunzi.

Nipashe imebaini kasoro hiyo ambayo sasa imeshabeba sura ya adha ya kisaikolojia kwa wanafunzi wenyewe, pia wazazi na walezi, ni pamoja na baadhi ya wanafunzi wanaokabiliwa na mitihani kukalishwa darasani wakifundishwa kuanzia alfajiri hadi usiku.

Pia, adha hiyo ya muda wa ziada inagusa kufutwa kinyemela kwa mapumziko ya wikiendi, siku ya Jumamosi na baadhi ya shule hata Jumapili, kufanywa kuwa za mahudhurio darasani.

Vilevile, gazeti hili limebaini mabadiliko hayo ya kinyemela ambayo yanaenda katika mfumo mithili ya 'kifurushi maalumu' kwa wanafunzi wanaokabiliwa na mitihani, wakiwamo wa darasa la sita, wameanzishiwa tuisheni za lazima, kabla hawajahamia bweni.

Dodosa za Nipashe katika shule hizo zaidi ya 10, zilipata majibu ya mpango wa muda wa ziada unatokana na kufidia miezi mitatu (wiki 13 au wastani saa 78), ambao watoto hawakuwapo masomoni kutokana na mlipuko wa maradhi ya corona, Machi mwaka jana.

Katibu Mkuu wa Umoja wa Wamiliki wa Shule na Vyuo Binafsi (TAMONGSCO), Benjamin Nkonya, akizungumza na gazeti hili, anatetea nyongeza ya muda huo ni kufidia muda uliopotea wa masomo kutokana na adha ya corona.

"Mwanafunzi anatakiwa kukaa siku 194 kwa mwaka, zimepungua mwaka huu kutokana na corona, hii inafidia siku zilizopungua miezi mitatu.

"Wazazi wakubaliane na hiyo hali, hata kulipa ada yote mbali na shule kufungwa sababu huduma zilienndelea kwenye shule mfano ulinzi, maji," alisema Nkonya.

Hata hivyo, serikali iliagiza shule zote kuongeza muda wa saa mbili za masomo darasani kufidia muda uliopotea wanafunzi walipokuwa nyumbani.

Katika kipindi cha miezi sita ambacho walihudhuria masomo kuanzia Juni 29 mwaka jana hadi Desemba 18, ambayo inamaanisha kuondoa likizo fupi ya zaidi ya wiki moja, Agosti mwaka jana, wanafunzi wamehudhuria darasani kwa wastani wiki 22.

Kwa kuzingatia mahudhurio shuleni ya siku tano kwa wiki, wanafunzi wamekaa darasani kwa siku 110, ambayo kila siku ya masomo walikuwa na saa mbili za ziada inayowapa jumla ya saa 220 wakati zilizopotea kwa corona zilikuwa saa 78, hivyo kuna ziada isiyopungua saa 140, sawa na wiki 20.

**HALI ILIVYO**

Uchunguzi wa Nipashe, uliozuru katika shule mbalimbali za wilaya za Kinondoni, Ubungo, Ilala na Temeke, umebaini msukumo mkuu nyuma ya pazia kwa tishio hilo la kiafya kwa wanafunzi, ni ushindani wa kibiashara.

Baada ya kubainika ufaulu ndiyo mvuto mkuu wa soko kwa shule, nazo kutokana na ushindani mkubwa uliopo, zimejikuta zikitumia mbinu kwa mfumo wa kuigana kibiashara, zikijitutumua kutafuta mafanikio ya wanafunzi wao ili wauzike.

Uchunguzi wa Nipashe katika baadhi ya shule zilizoko maeneo ya Ubungo, Kimara, Ukonga, Mbezi Beach, Tabata, Segerea na Mbagala, umebaini wanafunzi wengi wa darasa la saba na la nne wamekuwa wakiingizwa darasani kuanzia alfajiri hadi kati ya saa mbili na saa tatu pasipo kurudishwa bwenini.

Shule nyingi zimegundulika kuwalazimisha wanafunzi wa madarasa yanayokabiliwa na mitihani, zaidi darasa la nne na la saba, pia kidato cha pili na cha nne kuhamishiwa mabwenini kwa malipo ya ziada maradufu.

Ni hatua ambayo baadhi ya wazazi waliohojiwa na Nipashe, akiwamo Bryson Eliezer na Hilda Mosha (majina ya watoto wao na shule wanakosoma tunayo), wamethibitisha wameshawishiwa kupeleka bwenini watoto wao, ili wakasaidiwe kwa karibu kitaaluma, pasipo kuwekwa wazi mengine yanayojiri kuhusu ratiba.

Uchunguzi wa wiki kadhaa umegundua kwamba, katika ratiba ya mabwenini kwa shule nyingi, wanafunzi huanza rasmi masomo kati ya saa 11:30 na saa 12:00 asubuhi na ratiba hiyo ya darasani inagota kati ya saa mbili na saa tatu usiku.

Baadhi ya walimu waliifahamisha Nipashe kwamba, katika ratiba hiyo inayofanana kwa shule nyingi, kabla ya kuanza masomo, watoto hupatiwa uji na kisha saa nne asubuhi hupumzika nusu saa kwa ajili ya kunywa chai pamoja na wenzao wanaojumuika masomoni (wanaotoka nyumbani na wa bweni wenzao).

Aidha, ratiba zinaelekeza wanafunzi kupumzishwa mchana kwa saa nzima kati ya saa sita na nusu na saa nane, kwa ajili ya mlo na kisha wanarejea darasani, hadi jioni saa 12, wanapopumzika tena kwa nusu, wakipatiwa uji kabla ya kurudu tena darasani kwa saa mbili hadi tatu.

Hivyo, kwa kuzingatia ratiba hiyo ambayo mwanafunzi anakuwa katika ratiba za kishule kwa saa 14 hadi 15, ukiondoa mapumziko, muda kamili anaokabiliana na chaki za mwalimu darasani ni jumla ya saa 12 hadi 13 kwa siku.

**MAELEKEZO YA KISERIKALI**

Wakati kuna uhalisia huo unaotawala katika shule binafsi, ni ratiba inayopingana na maelekezo kutoka Mtaala wa Elimu ya Msingi wa Mwaka 2007, unaoweka wazi muda wa kusoma au kujifunza kwa aliyeko

Inaendelea Uk. 5

RIPOTI MAALUM

Inatoka Uk. 4

# Darasa la saba na la nne wakaa darasani saa 14, alfajiri hadi giza

kuanzia darasa la tatu hadi la saba, ukomo wake ni saa sita kwa siku.

Vilevile, serikali inaelekeza kwa wanafunzi walioko katika madarasa ya kwanza na la pili, wasizidishe saa tatu na nusu (3½) kila siku.

Vivyo hivyo, serikali inaelekeza kila mwaka wa masomo utakuwa na mihula miwili itakayokuwa na majuma 21 kwa kila muhula.

Hiyo inamaanisha kila muhula utakuwa na jumla ya siku 147, ambazo ni sawa na wastani wa miezi mitano kasoro siku kadhaa.

Ni mgawanyo wa mapumziko ya wanafunzi unaojenga maana ya kwamba, walau kila baada ya muhula mmoja, mwanafunzi anapaswa kupewa mapumziko yasiyopungua mwezi.

Vivyo hivyo, kwa mujibu wa ratiba ya siku rasmi za kufanya kazi, Jumamosi na Jumapili ni siku ambazo mwanafunzi hapaswi kuingizwa darasani.

Hali kadhalika, ikirejewa maagizo ya mwanafunzi wa darasa la tatu hadi la saba, anatakiwa kukaa muda wa saa sita akisoma na kujifunza, kwa anayeingia asubuhi walau hadi saa tisa muda wake utakuwa umeisha, tena kwa maelekezo ya kati ya Jumatatu hadi Ijumaa.

Serikali inaelekeza kila wiki madarasa ya tatu hadi saba, ambayo yanaangukia kwenye makundi ya mitihani, yatakuwa na jumla ya vipindi 42 vyenye dakika 40 kila kimoja.

Lakini, kwa kile Nipashe imekibaini, ufundishaji umefikisha siyo chini ya vipindi 84 hadi 90 kwa wiki.

Ni mageuzi ya kinyemela yanayoendelea katika baadhi ya shule, huku mfumo wa kiserikali ukiwa na wasimamizi wa elimu, waliogawanywa mahsusi kwa shule za msingi na sekondari.

Mgawanyo huo unaangukia katika kuwapo maofisa elimu kata, ngazi ya wilaya, mkoa na katika wizara yenye mamlaka ya elimu wakiwapo viongozi wa ngazi tofauti pamoja na Kamishna wa Elimu.

**KUTOKA KWA WAZAZI**

Akizungumza na gazeti hili, mzazi aliyejitambulisha kwa jina la Bryson Eliezer, alisema, mwaka huu watoto wake wawili, mmoja akisoma darasa la nne na mwingine la saba, wanahitajika kukaa shule ya bweni kulingana na maagizo ya shule wanayosoma.

"Wanangu wanatakiwa kukaa 'boarding' (bwenini), walimu wametuambia wazazi kuwa itawasaidia kumudu mitihani ya kitaifa. Lakini, wakati ninawaandikisha hakukuwa na utaratibu huu, kwamba mwaka fulani watahamia shuleni na ada inaongezeka," anasema Eliezer.

Pia, anathibitisha kuwapo ongezeko la ada kwa ajili ya bweni, malipo ya tuisheni ambayo kila mwanafunzi anatozwa kati ya Sh. 10,000 hadi Sh. 20,000 kwa mwezi.

Mzazi mwingine, Hilda Mosha, mkazi wa Mbezi Beach, Dar es Salaam, anasema shule anayosoma mtoto wake aliyepo darasa la nne



Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Profesa Joyce Ndalichako.

awali alilipia kiasi cha Sh. 1,500,000 na hivi sasa analazimika kulipa fedha nyingi zaidi.

"Kila mwezi Sh. 10,000 ninalipia, zidisha kwa miezi ya mwaka mzima, bila hiyo fedha watoto wanarudishwa nyumbani," anasema Hilda.

**SHIDA YA AFYA**

Daktari wa Binadamu, Pedro Pallangyo, akizungumza na gazeti hili, anasema kiafya saa za kukaa darasani kwa mtoto aliye shule ya msingi zisizidi 12 kwa siku.

"Kila kitu kina kipimo chake, saa 12 kwa mtoto wa shule ya msingi, hapana! Ubongo hauwezi kupokea kwa saa zote hizo," Dk. Pallangyo anatoa hadhari.

Katika hoja hiyo, Mtaalamu wa Lishe, Theresia Thomas, msisitizo wake ni kwamba kadri mwanafunzi anavyotumia muda mrefu katika masomo darasani, pia atahitaji chakula kilicho na nishati ya kutosha kipindi cha mapumziko.

"Kikubwa, nishati lishe inahitajika kuzingatiwa kwa mtoto yeyote. Iwapo mzazi ataona ni vyema akamfungashia mtoto wake juisi au matunda, ili akipata muda ale, muda wa mapumziko itafaa na si kusoma saa nyingi bila mlo, uelewa unachangiwa na lishe," anasema Theresia.

Mtaalamu wa Saikolojia Tiba, Saldin Kimangale, anasema kumrundikia mtoto mambo mengi, kunaangukia kupata msongo wa mawazo na hofu, inayomwondolea hamasa ya kufurahia masomo.

"Kumjazia mtoto mambo mengi na hasa ratiba zao za shule kiasi cha kukosa wakati wa kucheza na kufurahi, ni kasoro katika malezi bora," anaonya.

Mtaalamu huyo anataja athari anazoweza kuzipata kutokana na kujaziwa mambo mengi kwa wakati mmoja, ni pamoja na kupoteza vipaji na ubunifu alivyonavyo.

"Afya ya mwili ya mtoto pia huathirika, na kama tujuavyo afya ndiyo rasilimali na mtaji wa kila tunachofanya," anakumbusha mtaalamu huyo.

**TAMONGSCO**

Katibu Mkuu wa TAMONGSCO, Benjamin Nkonya, mbali na hoja yake ya msingi, kuhusu kufidia muda utokanaona shule kufungwa kipindi cha corona, anaeleza:

"Kumwacha mwanafunzi na ukakaa naye saa chache, kuna athari kubwa zaidi kuliko saa nyingi. Ukikaa naye zaidi atafaulu, nina imani waliokaa na kufanya hayo, ni watu wa elimu, wana utaalamu wa kutosha."

Anatetea wanafunzi wa darasa la nne na la saba kuhamishiwa bwenini kwamba ni hoja ya msingi, kwa sababu wataingizwa darasani kwa muda unaotakiwa.

**WAZIRI ELIMU**

Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Profesa Joyce Ndalichako, hivi karibuni katika mkutano mkuu wa mwaka wa Wakuu wa Shule za Sekondari Tanzania Bara (TAHOSSA), ana hoja inayojibu kinachojiri:

"Kumeibuka tabia ya shule imesajiliwa kama ya kutwa mara ya muda kidogo inakuwa ya bweni bila hata kufuata taratibu, eti tu kwa sababu imejenga 'kajengo kamoja' na kukaita bweni.

"Darasa la mitihani ndiyo walimu wanaona ndilo la kumjazia mtoto vitu vyote, unakuta hata shule hawafungi, eti tu kwa sababu ya mitihani. Kwa nini hali hiyo isiwe toka madarasa mengine ya chini na siyo kusubiri wakati wa mitihani?"

Agizo la Profesa Ndalichako, ambaye ni mtaalamu bingwa wa mitaala, anazitaka shule binafsi zirejee na kuhakikisha hazitoki nje ya kanuni za usajili wao na kuacha tabia ya kujichukulia hatua bila kuishirikisha serikali.

Vivyo hivyo, alielekeza kidole cha kung'aka dhidi ya tabia za shule kusubiri darasa la mitihani, ndiyo wanahamia utaratibu wa kuwalimbikizia masomo wanafunzi.



Wanafunzi wa darasa la saba wakiwa kwenye chumba cha mtihani wa taifa.

# MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## *Ongezeko la mapato TRA ni la kupongezwa, juhudi ziongezwe*

**MAMLAKA** ya Mapato Tanzania (TRA), imemaliza mwaka 2020 kwa kishindo baada ya kutangaza kuwa katika mwezi uliopita, imekusanya Sh. trilioni 2.088, hivyo kuvuka lengo lake la kukusanya Sh. 2.072.

Pamoja na kuvuka lengo hilo, kiwango hicho cha makusanyo kimevunja rekodi si tu tangu kuingia madarakani kwa serikali ya awamu ya tano bali tangu kuanzishwa kwa mamlaka hiyo zaidi ya miaka 25 iliyopita.

Makusanyo hayo pia yanaonyesha kwamba kumekuwa na kupanda kwa viwango vya ukusanyaji wa mapato kila mwezi kuanzia Julai hadi mwezi uliopita. Katika mwaka wa fedha wa 2020/21, takwimu zinaonyesha kwamba Julai, mwaka jana, mamlaka ilikusanya Sh. trilioni 1.2.

Ongezeko hilo liliendelea kupanda Agosti hadi kufikia Sh. trilioni 1.3 na kuchupa Septemba na kufikia Sh. trilioni 1.7 kabla ya kushuka Oktoba na Novemba hadi Sh. trilioni 1.3 kila mwezi.

Kwa hatua hiyo, TRA imeonyesha dhamira ya dhati ya kukusanya mapato kama inavyotakiwa ili kuiwezesha serikali kutekeleza miradi yake ya maendeleo pamoja na matumizi mengine kwa kutumia zaidi fedha za ndani. Sambamba na hayo, ongezeko la makusanyo hayo litasaidia kulipa sehemu ya madeni ya ndani na ya nje.

Kamishna Mkuu wa TRA, Dk. Edwin Mhede, akizungumzia mafanikio hayo juzi, alisema hatua hiyo ni kutokana na wafanyakazi kufanya kazi kwa kujituma na weledi pamoja na kupata ushirikiano mzuri kutoka kwa walipakodi.

Pamoja na hayo, alisema mafanikio hayo kwa kiasi kikubwa yamechangiwa na mwitikio wa walipakodi na kusisitiza kwamba kama wasingekuwapo na mwitikio ungekuwa mdogo, ni dhahiri kwamba wasingevuka lengo la kuvunja rekodi hiyo.

Si hiyo tu, hatua hiyo pia inadhihirisha kwamba elimu inayotolewa kwa walipakodi inaeleweka vilivyo. Pia hali hiyo inaonyesha kwamba kuna ushirikiano mkubwa baina ya TRA, walipakodi na wadau wengine.

Hatua iliyofikiwa na TRA katika kuvunja rekodi ya ukusanyaji mapato pamoja na ongezeko la kila mwezi katika malengo yake, ni ya kupongezwa kwa sababu inatia moyo kwamba nchi inaweza kufanya mambo yake ya maendeleo kwa kutumia fedha za ndani kama Rais John Magufuli ambavyo amekuwa akisisitiza.


Pamoja na pongezi hizo, mamlaka hiyo bado ina jukumu zito la kuhakikisha inaongeza kasi ya ukusanyaji wa mapato kupitia vyanzo mbalimbali pamoja na kuendeleza kuziba mianya ya ukwepaji kodi. Moja ya mbinu ambazo TRA inapaswa kutumia ni kuhakikisha matumizi ya mashine za kielektroniki za kutolea risiti (EFD) yanasisitizwa na kusimamiwa ipasavyo kwa kuwa kutotumia vifaa hivyo, kunasababisha kuvuja kwa mapato.

Katika kuhakikisha hilo linafanikiwa, TRA haina budi kuwabana wafanyabiashara wanaoshindwa kutii maagizo ya kutumia mashine hizo sambamba na kuwachukulia hatua baadhi ya watumishi wake wasio waaminifu ambao wamekuwa wakidaiwa kushirikiana na wakwepa kodi kuikosesha serikali mapato.

Sambamba na hilo, serikali kwa kushirikiana na TRA, haina budi kuweka mkazo zaidi katika kodi ya zuio (withholding tax) katika pango la nyumba hasa zile za kupangisha kwa ajili ya makazi pamoja na biashara.

Kwenye eneo hilo baadhi ya wamiliki wa nyumba, hasa wale binafsi, wamekuwa wakifanya udanganyifu wa thamani ya fedha wanazotoza katika upangishaji na matokeo yake serikali kukosa mapato. Ni imani kuwa kama mkazo utawekwa katika eneo hilo, ongezeko la mapato litaendelea kuwa juu.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji:** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

## *Mwaka 2021 uwe wa Tanzania bila vifo vitokanavyo na Ukimwi*

Na Sabato Kasika

**TANGU** Ukimwi ulipoingia nchini mwanzoni mwa miaka 80, umeangamiza watu wengi duniani huku pia juhudi mbalimbali zikifanyika kwa ajili ya kukabiliana na ugonjwa huo ambao bado tiba yake haijapatikana.

Serikali ya Tanzania na wadau wake, kama zilivyo nchi zingine duniani, imefanya jitihada ambazo kwa kiasi fulani zimeanza kuzaa matunda ambayo ni vyema kila Mtanzania akashiriki kuziendeleza anapoingia katika mwaka huu wa 2021.

Kwa mafano, serikali imeimarisha huduma za tiba ikiwamo matumizi ya dawa za kufubaza virusi vya Ukimwi (ARV) pamoja na kutoa elimu ambayo imesaidia watu kutambua umuhimu wa matumizi ya dawa hizo. Hatua hiyo imepunguza vifo vinavyotokana na maambukizo ya virusi vya Ukimwi (VVU) nchini kutoka 85,000 mwaka 2011 hadi 25,000 mwaka 2019. Hali hii inaonyesha kwamba kuwa huenda vikaisha iwapo juhudi hizo zitaendelea.

Upunguaji wa vifo hivyo unaelezwa na Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, katika maadhimisho ya Siku ya Ukimwi Duniani yaliyofanyika kitaifa mkoani Kilimanjaro, Desemba mosi mwaka uliopita. Alibainisha kwamba elimu ya matumizi ya ARV imechangia watu kuelewa na kuanza kuizingatia na maelezo hayo ya Waziri Mkuu ni kama yana mwezi mmoja tangu ayatoe kwa umma wa Watanzania na kuhimiza umuhimu wa elimu.

Elimu ya kujua matumizi sahihi ya dawa za kufubaza makali ya Ukimwi ni ya muhimu kutokana na ukweli kwamba baadhi ya watu wamekuwa wakikataa kutumia kutokana na sababu mbalimbali. Wako wanaoona aibu, wengine kuona usumbufu kunywa na pia wako ambao wanaamini kwamba wakienda katika nyumba za ibada wanaweza kupona bila kutumia ARV.

Lakini ni vyema kile ambacho kinaelekezwa na serikali au wataalamu wa afya kikazingatiwa ili kila aliyeathirika anywe dawa husika ili kumsaidia kuwa salama zaidi na kuendelea kupunguza vifo vitokavyo na Ukimwi. Wakati huu ambao tumeanza mwaka mpya wa 2021, kila mmoja hana budi kuzingatia hilo, ikiwamo kuepuka maambukizo na kama bahati ambayo mtu atakuwa ameambukizwa, awe tayari kutumia ARV.

Katika kuhakikisha huduma za afya zinaimarishwa, serikali imekuwa ikijitahidi kujenga zahanati, vituo vya afya na hospitali ili zitoe huduma kwa Watanzania katika maeneo mbalimbali nchini. Mbali na hilo, Tanzania ina Sheria ya Ukimwi iliyopitishwa na Bunge mwaka 2008 inayoelekeza mambo mbalimbali muhimu yanayohusu mtu aliyeambukizwa VVU na jinsi anavyotakiwa kufanya.

Sheria hiyo ni mahsusi ili kuzuia maambukizo ya VVU, kuendeleza na kutunza afya ya jamii na inatoa mwongozo wa huduma inayotakiwa kwa watu walioambukizwa au kwa wale walio katika hatari ya kupata maambukizo.

Pia inataja haki za mtu anayeishi na VVU kuwa ni kupata huduma za afya ya mwili na akili kwa kadri ya ubora unaohitajika, kupata matibabu sahihi ya magonjwa nyemelezi na kupata haki zote alizonazo binadamu mwingine yeyote ambaye hajaathirika. Vilevile sheria hiyo inataja wajibu wa mtu anayeishi na VVU kuwa ni kulinda wengine wasipate maambukizo ya ugonjwa na kushiriki na kuchangia katika maendeleo ya kisayansi na mafanikio yake.

Wizara husika inatakiwa kuhakikisha ARV pamoja na huduma nyingine muhimu za afya na dawa vinapatikana, na kwamba mtu yeyote haruhusiwi kumbagua au kumnyanyasa mwenye VVU. Binafsi ninaamini kwamba, kila mmoja akizingatia jinsi sheria hiyo inavyotaka, hakutakuwa na njia ya mkato ya kukabiliana na VVU, badala yake, aliyembukizwa atatumia ARV, kwa ajili ya kufubaza virusi hivyo.

Mwaka 2021 uwe ni mwanzo wa kila aliyeambizwa VVU kutumia dawa husika ili kupungyuza vifo huku wakitambua kuwa makali ya ugonjwa huo mwilini hufubazwa kwa dawa za kufubaza virusi.

Lakini, wataalamu wa afya wanabainisha kuwa, kwa ufubazaji wa VVU, hufanya watu wenye virusi hivyo kuishi kwa muda mrefu kuliko wale ambao hawapati matibabu hayo.

Hivyo wale ambao walikuwa hawajagundua hilo, na ikiwezekana, mwaka huu uwe wa mabadiliko ili hatimaye ifikie kwamba, Tanzania bila vifo vitokanavyo na Ukimwi inawezekana.

SAFU

## FIKRA MBADALA

# CHADEMA igeni mfano wa ACT-Wazalendo



Nkwazi Mhango, Canada

**Kimsingi, kilichofanyika Zanzibar ni kuheshimu Katiba ambayo inatamka wazi kuwa chama kitakachokuwa cha pili kitapewa nafasi ya umakamu wa kwanza wa Rais na viti kwenye Baraza la Mawaziri kulingana na asilimia ya ushindi wa chama husika.**

UCHAGUZI mkuu uliopita ulijaa vimbwanga, visasi, visingizio hata vitisho hasa baada ya kutangazwa matokeo ya uchaguzi ambapo Chama Cha Mapinduzi (CCM) kilishinda kwa kishindo kwa aslimia 84 urais na kuzoa viti karibu vyote, huku upinzani ukiambulia viti viwili tu upande wa Bara jambo ambalo halijawahi kutokea tangu kuingia mfumo wa vyama vingi.

Japo ni nje ya mada ya leo, washindi wa viti viwili tu vya upinzani Bara ni wanawake mmoja toka CHADEMA na mwingine toka CUF.

Hivyo, unaweza kusema kuwa uchaguzi wa mwaka huu umeutia ufa mfumo dume na imani kuwa kinamama hawawezi siasa za ushindani wakati wanaziweza kama walivyodhihirisha. Kwani, kwenye bunge lililoanza hivi karibuni, upinzani kwa upande wa Bara hautakuwa na mwanamume hata mmoja.

Ushindi wa kinamama hawa ambapo wanaume wote walishindwa uwahamasishe kinamama wengi kushiriki nafasi za kuchaguliwa na kuachana na kutegemea nafasi za viti maalumu ambazo sasa ziko zinawagombanisha wao kwa wao na vyama vyao kwa baadhi ya vyama.

Kimsingi, viti hivi viwili vinakomesha matusi na upuuzi kuwa kinamama siyo thabiti kisiasa kiasi cha kutegemea viti vya dezo. Kama kinamama wameweza kumzaa kila mmoja wa binadamu wote duniani, watashindwa nini kumwongoza? Nayapongeza majimbo yaliyowachagua hawa kinamama wawili waliovunja rekodi ya kuwachakaza wanaume waliotoka kapa kiasi cha sasa kuanza hata kuwawekea mizengo kwenye viti walivyoshinda kihalali na kwa kuvuja jasho.

Hata hivyo, pamoja na upinzani kusimama kidete kupinga matokeo, wapo waliofanya kile ambacho Waingereza huita Road to Damascus kwenye kisa cha Biblia ambapo hasidi mkubwa wa Yesu aliyekuwa akiua wanafunzi wake Paulo au Sauli 'alitokewa na sauti ya Bwana' akaamua kuslimu na kujiunga na kumfuata Yesu.

Chama cha ACT-Wazalendo tunakipongeza kwa ujasiri wake wa kuachana na msimamo ambao ulikuwa hasi hasa pale kilipokaribishwa kujiunga na SUK Visiwani kikaanza kugoma goma na mwisho wake kikaamua kuingia hasa ikizingatiwa kuwa kama si Katiba ya Zanzibar kukibeba, hapakuwa na namna au stahiki ambapo chama kilichoshindwa kingeingia kwenye serikali.

Kimsingi, kilichofanyika Zanzibar ni kuheshimu Katiba ambayo inatamka wazi kuwa chama kitakachokuwa cha pili kitapewa nafasi ya umakamu wa kwanza wa Rais na viti kwenye Baraza la Mawaziri kulingana na asilimia ya ushindi wa chama husika.

Hivyo, kitendo cha awali cha ACT-Wazalendo kukataa mwaliko wa kujiunga na SUK ilikuwa ni kinyume na Katiba. Sasa ACT-Wazalendo wamo ndani, hakuna tena ubishi kuwa wametekeleza matakwa na maagizo ya Katiba ya Zanzibar. Pamoja na yote, tunawapongeza kwa hili.

Maana hakuna mgogoro usio na mwisho hasa muamuzi mwenyewe wanapokuwa ni wananchi walioamua kuichagua CCM.

Hata hivyo, kwa upande wa Bara ambapo Katiba ni tofauti na Visiwani iko wazi kuwa chama kitakachoshinda kitaunda serikali bila kulazimika kikatiba na kisheria kuwashirikisha walioshindwa, hali ni tofauti. Kama tulivyoeleza kwenye utangulizi, upinzani, pamoja na kushindwa kwa kishindo wazi wazi, bado haujaitambua serikali ya CCM ambacho kilishinda uchaguzi kihalali.

Wakati ACT-Wazalendo iliyochukua nafasi ya pili Visiwani ishapeleka wateuliwa na wachaguliwa wake, Bara ambako nafasi ya pili ilishikiliwa na CHADEMA, bado wahusika wanavutana. Hadi tunaandika wabunge 19 wa viti maalum waliochaguliwa na Baraza la Wanawake CHADEMA (BAWACHA), licha ya kuamriwa na chama wasishiriki bunge, walitimuliwa uanachama kwa kukubali kuapishwa na Spika wa Bunge kwa mujibu wa sheria.

Hii maana yake ni kwamba CHADEMA wameamua kupinga Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (1977) inayotamka wazi kuwa mshindi wa uchaguzi mkuu ndiye ataunda serikali bila kulazimika kuwakaribisha wapinzani tena walioshindwa kama ilivyo Visiwani ambako Katiba ilifanya hivyo kutokana na mazingira ya huko na migogoro isiyo na mwisho iliyowahi kuleta maafa kule.

Japo kususa kutuma wawakilishi wake ambao wanaona hawakufuata utaratibu ni haki yao kama chama, ila si haki yao kudharau maagizo ya Katiba kama wananchi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na taasisi ya umma ambayo uhalali wake unatoka kwenye Katiba ile ile wanayopinga maelekezo yake kama watashikilia msimamo wa kutotuma watu wake bungeni. Pamoja na kuwapo wanaoona kama kilichotokea Visiwani ni matokeo ya siasa za sura badala ya sera na mvuto wa ulaji kwa wahusika, bado tunawapongeza kwa kukubali maelekezo ya katiba.

Kwani nani asiyetaka ulaji tena kama ni wa dezo kwa mtu au chama kilichoshindwa vibaya?

Tumalizie kwa kuwataka CHADEMA wafikiri upya hasa ikizingatiwa kuwa kushiriki bunge ni amri ya kikatiba na si ya utashi. Wamalize mgogoro na kinamama wao watoe mchango kwenye uendeshaji wa nchi kwa mujibu wa Sheria na Katiba.

## MADONGO YA MGAGAGIGIKOKO

# Tukichekea wanasiasa tutavuna mabua



Na Joseph Kulangwa

**Magereza ambao husubiri kupokea wahalifu kutoka Polisi, nao hawapendi kusikia nchi ina wahalifu, kwa kuwa wanawasumbua kuwahifadhi wakiwa mahabusu au magerezani, lakini wasipokuwapo, askari Magereza watafanya kazi gani? Je, wasipofanya kazi itakuwaje?**

MUUZA jeneza siku zote huchukia kifo, lakini hukasirika majeneza yake yasipopata soko. Hujiuliza kulikoni, na huombea apate wateja ili apate riziki, kwa sababu asiyefanya kazi na asile na asiyekula afe.

Mganga wa kienyeji siku zote huchukia kifo na magonjwa, lakini hukasirika sana asipopata mgonjwa, kwa sababu atakosa riziki yake. Naye atajiuliza kulikoni asipate wateja, na huishia kuichukia hospitali.

Na huyu huenda mbali zaidi, akiona amekosa wateja atafanya juu chini awatengeneze, kwa kuwaroga, ili wamtafute wampelekee riziki. Waswahili husema mbwa anakula miguuni kwake, huku mbuzi akila kwa kadri ya urefu wa kamba yake.

Nchi ikiwa na usalama wa raia na mali zao pia, yawezekana polisi wakakosa kazi, na wakikosa kazi watakosa riziki. Sasa wakikosa riziki itakuwaje, kwa sababu asiyefanya kazi hatakula na asipokula atakufa.

Polisi wanachukia sana uhalifu, wanachukia wanaohatarisha usalama wa raia na mali zao, lakini wakikosekana watu hawa wanaoitwa wahalifu, ina maana polisi hawatafanya kazi.

Magereza ambao husubiri kupokea wahalifu kutoka Polisi, nao hawapendi kusikia nchi ina wahalifu, kwa kuwa wanawasumbua kuwahifadhi wakiwa mahabusu au magerezani, lakini wasipokuwapo, askari Magereza watafanya kazi gani? Je, wasipofanya kazi itakuwaje?

Halikadhalika wauza dawa za kurefusha maisha kwa wagonjwa wa Ukimwi, nao hawapendi kuona watu wanapoteza maisha yao kwa ngono zembe, lakini itakuwaje kusipokuwa na waathirika wa Ukimwi, dawa hizo atauziwa nani?

Hivi mnadhani wauza barakoa walifurahi Uviko-19 ulipotoweka nchini ghafla? Fikiria barakoa la kitenge utalivalia wapi kama korona haipo? Nawe unayelishona utamuuzia nani?

Kwa hiyo haya mambo yapo tu na yanategemeana kwa kiasi fulani, tutayachukia, lakini tutayapenda pia. Hatupendi watu wapoteze maisha, lakini kumbe wakipoteza maisha pia ni fursa kwa wengine. Hebu fikiria wachimba makaburi!

Ndiyo sababu wanasiasa hata siku moja hawatakubali wananchi wa kawaida waondokane na ujinga kwa asilimia 100, kwa sababu kwa kufanya hivyo, watagundua njama zao chafu za kujipatia maslahi kupitia migongo yao.

Wanasiasa watapanda majukwaa kudanganya wananchi; tutakufanyieni hiki na kile ili kukuondoleeni kero na adha hizi na zile, lakini hatimaye hakitafanyika kabisa au nusu, ili wananchi waendelee kuogelea kwenye dimbwi la matatizo. Uogeleaji huo ni wananchi kuendelea kuishi wakitegemea ahadi hewa, huku wanasiasa nao wakitegemea kura ili waendelee kula na kushiba migongoni mwa wananchi.

Kulithibitisha hili, ni kufuatilia kampeni na kusikiliza ahadi na kisha utekelezaji wa ahadi, ndipo utabaini kwamba kumbe wanafurahia raia kuumia ili waendelee kuula.

Sikiliza mijadala na maswali bungeni, hutakosa kusikia maswali ya barabara ile, jengo lile, mioundombinu ile, ziwa lile, mto ule na bwawa lile. Ili mradi ni mambo yale yale yataulizwa vile vile katika kila kikao na mkutano na kujibiwa vile vile na kupongezana na siku kusonga mbele.

Maswali na majibu ya wanasiasa wao kwa wao au kutoka kwa wananchi au kwa wanahabari, ni fursa ya kuaminiwa kushughulikia matatizo na ikiisha mitano, inatafutwa mitano mingine na maisha yanaendelea vile vile.

Inawezekana miaka mitano iliyopita, tuliwasikia wale wale wakitwambia yale yale, tukawachagua vile vile na maisha ya miaka mingine mitano yatakuwa yale yale na tutaendelea kuishi vile vile, tukiahidiwa ahadi zile zile. Muhimu ni amani na utulivu wetu tu.

Utakutana na mwanasiasa ambaye wakati wa uchaguzi hakuwa hivi, alikuwa mpole na mpiga magoti, mgalagala chini, akiomba kura yako ili akale, leo atataka wewe ndio umpigie magoti na ugalegale chini, ili akusikilize shida yako, akikusaidia haya, asipokusaidia shukuru Mungu pia.

Pengine miaka mitano hii ijayo, utakutana na mwanasiasa jeuri, atakayediriki kukushikia mjeledi, ili ukibiashana naye akulaze chini na kukucharaza, hata kama una mzuzu au sharubu. Lazima atataka akuonyeshe yeye ni nani na wewe ujitambue ni nani mbele yake. Ni wakati wa kuwasoma viongozi wetu na kuwakosoa pale tutakapoona hawaendi tutakavyo, wasijali yatakavyo matumbo yao wakibisha tuwasemee kunakohusika, tukisikilizwa haya, tusiposikilizwa tumshukuru Mungu.

**Alamsiki!**

## KONA YA UKWELI

# Kwa makusanyo haya TRA, hakika utegemezi kwa mabeberu utakwisha



Na Thobias Mwanakatwe

ULIPAJI kodi ni chanzo kikuu cha mapato ya kila nchi kwa ajili ya maendeleo ya kijamii, kiuchumi na hata kisiasa.

Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), juzi, ilitangaza kuwa imekusanya Sh. trilioni 2.088 kwa Desemba 2020 hivyo kuvuka lengo lililokuwa limewekwa. Lengo la makusanyo kwa mwezi huo lilikuwa Sh. trilioni 2.072.

Kiwango hicho cha makusanyo hakijawahi kufikiwa katika historia ya mamlaka hiyo tangu ilipoanzishwa mwaka 1996.

Hii ni hatua ya kupongezwa sana kwa Watanzania wote, walipakodi na TRA kwa kufanikiwa kukusanya kiwango hicho kikubwa. Hili ni jambo lenye kutia moyo sana na faraja kwa Watanzania wapenda maendeleo.

Baada ya TRA kutangaza makusanyo hayo, nilijipa muda nikaanza kupitia mapitio ya uchumi ya kila mwezi kutoka Benki Kuu ya Tanzania (BOT) kwa Desemba, 2020.

Ripoti hiyo inaonyesha kuwa kwa Oktoba, mwaka jana pekee, serikali ilikusanya takribani Sh. trilioni 1.682 kutokana na makusanyo yote ya kikodi na yasiyo ya kikodi. Kwa mujibu wa taarifa hiyo, makusanyo ya kikodi yalikuwa Sh. trilioni 1.295 na yasio ya kikodi yalikuwa Sh. bilioni 282.2, huku makusanyo kutoka serikali za mitaa kutokana na mapato ya ndani yakiwa Sh. bilioni 51.2.

Lakini tukienda kwenye matumizi ya serikali, kwa Oktoba 2020, ripoti hiyo (Monthly Economic Review) inaonyesha kuwa serikali ilitumia takribani Sh. trilioni 1.854, matumizi ya kawaida yakiwa trilioni 1.282 na matumizi kwenye miradi ya maendeleo ni Sh. bilioni 571.

Matumizi makubwa zaidi kwenye serikali yanakwenda kwenye mishahara ya watumishi wa umma ambapo kwa Oktoba, mwaka jana, yalikuwa takribani Sh. bilioni 601.7.

Pesa nyingine inatumika kulipa madeni na katika mwezi huo, serikali ilitumia takribani Sh. bilioni 192.4 kulipia madeni ya sasa na ya nyuma pamoja na riba.

Kwa maana hiyo, kwa Oktoba, mwaka jana, serikali ilitumia fedha nyingi zaidi ya Sh. trilioni 1.854 kuliko pesa tulizoingiza ambazo ni Sh. trilioni 1.628 kwa mwezi.

Kwa hatua ya TRA kufikia makusanyo ya Sh. trilioni 2.088 na kama kasi hii itaendelea hivi hivi kila mwezi, maana yake ni kwamba serikali itakusanya fedha nyingi zaidi kuliko matumizi kwa mwezi .

Hii itasaidia sana kwa nchi kupunguza mzigo wa kuendelea kukopa fedha kutoka kwenye taasisi za kimataifa za fedha na nchi wahisani kwa maana ya mikopo ya bei nafuu na mikopo ya kibiashara kutoka kwenye benki za kibiashara duniani.

Kwa tafsiri nyingine, TRA ikiendelea na kasi hii ya ukusanyaji mapato kwa kiwango cha juu, ni wazi kuwa mambo ya kuwategemea mabeberu kutusaidia fedha kwa ajili ya miradi ya maendeleo, tutaondokana nayo.

Kuwategemea mabeberu kumeziathiri nchi nyingi za kiafrika kwa sababu wanapokupa fedha au msaada, lazima wakupe na masharti makali ambayo usipoyafuata urafiki na wao unakuwa umekoma.

Lakini katika suala hili la mafanikio ya ukusanyaji mapato, ni wazi kwamba nchi itajitegemea na itaendesha mambo yake yakiwamo ya miradi ya maendeleo bila kutegemea wahisani na bila kuwapo masharti yoyote.

Kabla ya serikali ya awamu ya tano kuingia madarakani, makusanyo ya kodi yalikuwa hayazidi Sh. milioni 800 kwa mwezi, lakini baada ya Rais Dk. John Magufuli kukabidhiwa nchi, makusanyo yakaongezeka na kufikia zaidi ya Sh. Trilioni moja kwa mwezi, muda mfupi tangu ashike hatamu za uongozi.

Yako mambo mengi yaliyochangia kuongezeka kwa makusanyo ya mapato kama yaliyoelezwa na TRA, lakini kwa mtazamo wangu, suala la kuwadhibiti baadhi ya watendaji ndani ya TRA waliokuwa wakiendekeza rushwa na ufisadi, limeongeza kiwango hicho.

Ni wazi kwamba kabla ya serikali ya awamu ya tano kuingia madarakani, baadhi ya watendaji TRA walionekana kama wanaishi mbinguni kutokana na kuwa na fedha nyingi ambazo wamezipata kwa njia za rushwa.

Rungu la kuwadhibiti wala rushwa na mafisadi, haliku-washukia tu watendaji wa TRA bali pia baadhi ya wafanyabiashara ambao walizoea kukwepa kodi kwa kutoa rushwa kwa wakusanya kodi.

Hatua iliyofikiwa na TRA, inapaswa kupongezwa kwani imeonyesha dhahiri kwamba imedhamiria kuleta mapinduzi katika ukusanyaji mapato ili kuisaidia nchi kuepukana na utegemezi.

Ili kufikia azma hiyo na kuleta maendeleo ya kweli, nawahimiza Watanzania wote tulipe kodi kwa ajili ya maendeleo ya nchi yetu. TRA kama chombo chenye mamlaka ya dhamana ya kukusanya kodi, tuipe ushirikiano mkubwa kwani kwa hivi sasa ina watendaji wengi wanaochukia rushwa na ufisadi.

Nawatakia heri ya mwaka mpya, kipaumbele kiwe kulipa kodi.

**MUNGU IBARIKI TANZANIA,**
**MUNGU IBARIKI TRA**

**Kwa maoni na ushauri tuwasiliane katika barua pepe mwanakatwe2015@gmail.com au WhatsApp 0762-183666**

## DARASA LA NDOA

# Tambua maadui wa ndoa yako - 1



Na Mch.Dk. Enock Mlyuka

MAISHA ya urafiki, uchumba hadi ndoa hupitia mitihani mingi. Ikumbukwe kuwa, iwapo tulimshinda shetani wakati wa uchumba na katika maisha ya awali ya ndoa, tujue kuwa shetani alijipanga upya na kuanzisha mashambulizi. Safari hii anatumia mbinu mpya ambazo hatukuzijua awali. Mtu anajikuta ndoa yake inashambuliwa na maadui kutoka kila upande.

Kwa bahati mbaya, wengine wanajikuta hawana muda wa kutafakari chanzo halisi cha matatizo yanayotokea katika ndoa zao. Mara nyingi, wanandoa wengi huelekeza vyanzo kwa wengine.

Tafakari ambayo kila mwanandoa anawajibika kuifanya ni hii: "Katika magumu yanayoikabili ndoa yangu, chanzo chake ni nini? Je, mambo yapi ni kwazo kwa mwenzangu? Ni muhimu sana mtu kujiuliza kwanza kabla ya kutafuta ubaya kwa mwingine.

Ukweli ni kwamba adui wa kwanza wa ndoa ni mwanandoa mwenyewe kwa sababu zinazoelezwa sehemu inayofuata. Kwa maneno mengine, wafuatao ndio maadui wa ndoa;-

**UTOTO KATIKA NDOA**

Kuwa tegemezi, kuongozwa na kukosa uamuzi na kujisimamia. Wako waliooa au kuolewa, lakini hawana uamuzi kuhusu maisha yao ya ndoa. Wanajikuta mara nyingi wakitekeleza matakwa ya wazazi, ndugu au marafiki. Hali hii imesababisha matatizo makubwa katika baadhi ya ndoa.

Ujana mwingi katika ndoa

Kuendelea na aina ya maisha yale yale ya kabla ya ndoa. Mwanandoa anaishi kana kwamba hana ndoa, yaani, anashindwa kutofautisha aina ya maisha kabla na baada ya kuoa au kuolewa.

Wengi huendelea na tabia za ujanani; kukosa uaminifu; kutowajibika katika ndoa; na kukosa kujua thamani ya mwenzi.

Kunyimana tendo la ndoa

Ndoa nyingi zimesambaratika kwa sababu ya jambo hili. Ikumbukwe kuwa, Mungu hakumpa Adamu msaidizi wa kutazamana na kucheka tu. Alimpa msaidizi ambaye angejisikia faraja kwake; ambaye angempa joto kamili la mwili.

Kunyimana haki ya ndoa kwa sababu zozote zile, isipokuwa ugonjwa ni chukizo kwa Mungu. Wanawake au wanaume wengine wametumia miili yao kama silaha ya kukomesha wenzi wao kwa sababu ya makosa fulani. Hali hii ni chanzo mojawapo cha ubakaji na mimba zisizotarajiwa ndani ya ndoa.

**KAULI MBAYA**

Wanandoa wengine wametafuta wachawi wa ndoa zao, wakati wameziharibu wenyewe. Waswahili wanasema, 'Mvunja ndoa na mjenga ndoa ni mwanandoa mwenyewe.'

Wengi wameharibu ndoa zao kwa kutumia vibaya vinywa vyao. Mfano; kuwasema wenzi wao vibaya, kuwanenea maneno mabaya, kutukana na kuwashambulia kwa maneno yaliyochoma na kuumiza mioyo yao. Tukawadhalilisha kwa maneno na majina mabaya, hata kupelekea mtu kukata tamaa; midomo ikapiga, ikajeruhi na kuua. Ulimi umegeuzwa kuwa silaha ya maangamizi.

Chanzo cha vurugu katika ndoa nyingi ni namna wenzi wanavyotumia midomo yao litokeapo kosa fulani. Ugomvi mwingi uliosambaratisha ndoa nyingi ulitokana na kujibizana vibaya katika mambo ambayo yangemalizwa kwa maelewano. Kama watu wangejifunza kuchukuliana kwa upendo na upole kutokeapo kosa, kungeepusha migogoro isiyo ya lazima.

Maneno makali yamekuwa silaha ya kubomoa na kuua ndoa nyingi, hatimaye kusambaratisha familia nyingi. Wako wanawake, ambao huanzisha maneno yatakayo sababisha waume zao washikwe na hasira. Aidha, wako wanaume wengine wanaosifika kwa gubu. Mume anaongea na mkewe kana kwamba anaongea na kijakazi. Hawezi kumpa mke heshima yake. Kila wakati anaonesha dharau na kutokujali.

Hali hii huondoa amani ya moyo. Mtu hata awe na kila kitu kizuri katika maisha yake, lakini kama moyo wake hauna amani, moyo umejaa masononeko, hawezi kuwa na afya nzuri na utulivu. Hata kama chakula kitakuwa kizuri kiasi gani, kitakuwa kama sumu kwake. Nafsi imejeruhiwa, hivyo, anaona kila kitu ni kibaya.

Wanandoa wengine wameharibu ndoa zao kwa sababu ya kusikiliza maneno ya watu wa pembeni. Waswahili wanasema, yakuambiwa, changanya naya kwako. Ni muhimu kujifunza kuchambua na kuchuja mambo.

Si kila unaloambiwa na mtu linaweza kuwa ni kweli. Watu wana malengo na nia tofauti. Wanandoa wengi wamekaribisha migogoro na kuvunja ndoa zao kwa sababu ya kusikiliza maneno ya watu wengine waliodhani wanawatakia mema, kumbe ni wabaya wao. Ni wajibu wa kila mwanandoa kuilinda na kuitunza amani katika ndoa yake.

**WAZAZI**

Uchunguzi umeonyesha kuwa baadhi ya wazazi ni adui wa ndoa nyingi. Baadhi ya wazazi wamechangia kuvuruga na kuvunjika kwa ndoa za watoto wao badala ya kusaidia kuzidumisha. Mfano; katika kipindi cha Mimi na Tanzania, kilichorushwa na Channel Ten, kilitoa habari ya baba mmoja aliyekuwa ameoa na kujaliwa watoto watatu.

Yule baba alipata ajali ya gari iliyopelekea matatizo ya uti wa mgongo, kiasi cha kutoweza kutembea tena. Baada ya tatizo hilo kutokea, mke alimkimbia mumewe, kwa shinikizo la wazazi wake.

Wazazi wa mwanamke walimtorosha binti yao na kumwacha yule baba katika hali ya ugonjwa na watoto wake watatu.Thamani ya huyu bwana ilikuwa pale alipokuwa mzima wa afya na uwezo wa kufanyakazi; amepata matatizo, thamani yake imeisha hapo. Mke kamkimbia mume wake!

Wengine wananyanyasa na kuvuruga ndoa za watoto wao hasa inapotokea mwanamke hapati ujauzito. Matukio ya kusimangwa kwa mke na mama mkwe kwa maneno "unajaza choo" imejeruhi wengi.

Wengine wamediriki hata kwenda kwa waganga wa kienyeji kujaribu kuvuruga ndoa za watoto wao. Wazazi wengi wanajisahau kuwa ndoa ni taasisi huru inayojitegemea. Ni taasisi yenye mamlaka na utawala kamili. Wazazi wanaingilia ratiba na mipango ya Mungu.

**Dk. Mlyuka ni mchungaji wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) na Mkurugenzi Mtendaji wa Tanzania Marriage and Child Care Foundation (TaMCare), asasi inayojishughulisha na masuala ya ndoa, familia na malezi. Kwa maoni, mafunzo na ushauri wasiliana naye kwa: info@tamcare.or.tz au WhatsApp +255655865555.**

# MAISHA

JANUARI 3, 2021

Nipashe

Baba, Mama na Mwana

*Jumapili*




Ukurasa 10

## Usimwambie mtoto ‘usinijibishe’, msikilize



Ukurasa 15

## MAISHA NI NYUMBA

Dondoo za kukipamba chumba cha kulala



## HARUSI

Ukurasa 12



## NYWELE ZAKO TU ukiziachia utapendeza

Ukurasa 14

# Usimwambie mtoto 'usinijibishe', msikilize

**Na Moses Ismail**

KARIBU jamii nzima inaamini kuwa mtoto yeyote yule anayesemwa na wazazi wake kisha akajaribu kujitetea kwa kuelezea uhalisi wa jambo analosemwa, wakati mzazi bado anagomba, hana adabu.

"Haiwezekana mzazi aseme na wewe ufungue 'domo' lako, ni utovu wa adabu", anasema Mwajuma Mohammed mama wa makamo mkazi wa Kunduchi jijini Dar es Salaam.

Kwa malezi aliyokulia yeye Mwajuma anaamini kumjibu mkubwa, achilia mbali mzazi wako, ni utovu mkubwa wa adabu kwani adabu inafundisha kuwa mtoto lazima anyamaze pale anaposemwa na wazazi, hata kama hana kosa.

Mwajuma anasema ipo njia ya mtoto kukataa kosa lisilo lake, ila si kwa kujibishana na wazazi wake wakati anapomsema, anasema mtoto anaweza kumfuata mzazi wake baadaye na kumweleza ukweli juu ya jambo alilogombezwa kwa adabu tu.



Tabia hii ya kuwanyamazisha watoto na kutosikiliza utetezi wao ipo sana kwa jamii za Kiafrika, tabia na mila zetu zinatutaka kufanya hivyo, ili mradi tu wanaotuhukumu ni wazazi wetu au wakubwa zetu.

Hali hii inamadhara fulani ya kisaikolojia hasa ikiwa inatokea kwa mtoto mara kwa mara kwa sababu ni suala linalohusiana na hisia pamoja na mfumo wa kukubali mambo katika akili.

Madhara ya kwanza kujionyesha ni ile hali ya mtoto hujenga tabia ya woga hasa inapotokea kugombezwa kwenyewe kunakuwa kwa ukali na kupigwa.

Hili linaanza kwa mtoto kupenda kujitenga mbali na wazazi wake kila wanapokuwa kwenye eneo moja na kama wazazi ni wafanyakazi na wanarudi nyumbani jioni, mtoto atajificha hata chumbani kwake ili mradi tu wasionane.

Kinachofuata baada ya hilo ni mtoto pia atapoteza uwezo wa kuhifadhi kumbukumbu vizuri kama vile kushindwa kuelewa masomoni na atapenda kuwa mbali na nyumbani.

Hii ikizidi kwa muda mrefu mtoto anaweza akakumbwa na hali ya sononi, anaweza kujichukia yeye mwenyewe, kuchukia wazazi wake na mara kadhaa anaweza kuombea wazazi wake wafe ili awe huru.

Hali hiyo inaweza kuendelea mpaka ukubwani na anasihi sana wazazi kujenga urafiki baina yao na watoto wao na hata inapobidi kuwakanya basi wasitumie ukali kupita kiasi na pia wawape watoto nafasi ya kujieleza.

Kumzuia mtoto kujitetea, kutoa dukuduku lake moyoni na kumlazimsha kukubali kosa lisilo lake ni vitu vinavyomdhuru mtoto kiroho, kiakili na kimwili ingawa wazazi wengi wanadhani ndio adabu.

## NA HAMIS KIDAGO 0657 207168 QUIZ

**Comment t'appelles – tu?: Unaitwa nani?**
1. Soma dayolojia ifuatayo katika lugha ya Kifaransa na ujaze sehemu zilizokuwa wazi.

**Dayolojia**
Katika lango kuu la kuingia katika Shule ya Sekondari, baada ya likizo ya masomo kuisha, Raswiina na Sarah wanakutana na marafiki wapya.
Raswiina: Salut!
Sarah: .................
Raswiina: .................................................. ................. Sarah: Je vais bien, merci. Et toi?
Raswiina: ............................................... .................... Sarah: ................................ .......................................... Raswiina: Je m'appelle Raswiina.
Sarah: Moi, c'est Sarah. Je suis de Dodoma. Raswiina: Je suis ravi de te connaitre, Sarah.
Sarah: Moi de meme.
Sarah: Quel est le nom de ta copine?
Raswiina: Elle s'appelle Mariam. Elle vient de Kilimandjaro comme moi!
Sarah: Salut Mariam, je suis contente de faire ta connaissance!
Mariam: Je suis contente egalement de te connaitre, tu es sympathique!
Sarah anamuita rafiki yake mmoja wa darasani ambaye anakuja akikimbia.
Sarah: Je vous presente ma meilleure amie. Elle s'appelle Nathalie. Elle est francaise d'origine espagnole. Elle est en Tanzanie pour une annee. Elle habite dans ma famille. On est dans la meme classe.
Mariam et Raswiina: Nous sommes enchantees de faire ta connaissance, Nathalie! Nous te souhaitons la bienvenue dans notre lycee!
Nathalie: Moi aussi je suis heureuse de vous connaitre, vous etes tres gentilles!


**Maelezo ya kuzingatia**
**Jinsi ya kuuliza jina la mtu**
• Commenttut'appelles?– .............................................?(informal).
• Commentest-cequetut'appelles?– .. ..............................................? (informal).
• Commentvousappelez-vous?– .. ............................................................? (formal).
• Commentt'appelles-tu?-Unaitwa-nani? (informal).
• Comments'appelle-t-il?– Yeye(wakiume) anaitwa nani?
• Comments'appelle-t-elle?– Yeye(wakike) anaitwa nani?
• Quelestton-nom?–..............................................? (informal).
• Quelestsonnom?–Jinalakeninani?
• Quies-tu?–Weweninani?(informal).
• Quiest-elle?– ..............................................(wa kike)..................................?
• Quiest-ce?– ...........................................................?

**Jinsi ya kujibu (ukiulizwa unaitwa nani).**

! Je m'appelle Nathalie – ..................... .................................................... ....
! Il s'appelle Idd – Yeye (wa kiume) anaitwa Idd.
! Elle s'appelle Sulayhat – Yeye (wa kike) anaitwa Sulayhat.
! Mon nom est Beatrice (ou mon nom, c'est Beatrice) – .......................... .......................
! Son nom est John (son nom, c'est John) – Jina lake ni John.
! Moi, c'est Yusuph; elle, c'est Fadhila – Mimi ni Yusuph; yeye (wa kike), ni Fadhila.
! Je suis Benjamin – Mimi ni Benjamin. Jinsi ya kumtambulisha mtu.
"Je vous presente Monsieur Dupont, notre voisin – Na(ku/wa)tambulisha Bwana Dupont, jirani (wa kiume) yetu.
"Je te presente notre directrice – ... ................................................................ (wa kike).
"Je te presente mes amis: Farida, Erick et Mariam – Nakutambulisha marafiki zangu: Farida, Erick na Mariam.

## WATOTO

# PAKA RANGI




## CHEKA

JAMAA mmoja ambaye aliondoka kazini na kuaga anakwenda Dodoma baba yake mzazi anaumwa.

Alipoondoka alituma meseji kwa bahati mbaya kwa bosi wake.

**Jamaa:** Mpenzi wangu bosi wangu mnoko, ndio maana Mungu kamnyima sura kama boksi, nimemdanganya baba mgonjwa ili nije kwako.

**Bosi:** Eti!

Alichokifanya daktari

SWALI
Kaa anapatikana wapi?

# MAISHA NDIVYO YALIVYO

Na Flora Wingia



## Nahitaji mume wa ndoa, umri unakwenda sana, nifanyaje?

HERI ya Mwaka Mpya mpenzi msomaji. Sifa apewe Mungu wetu aliyetukubali tena kuingia mwaka huu 2021 kwa furaha kubwa. Kila mmoja wetu ana malengo na matarajio aliyojiwekea kuyafanikisha.

Yapo mengi ambayo yamkini hukuweza kufanikisha mwaka uliopita 2020, lakini sasa unamsihi Mungu yatimie. Wapo walioomba wapate watoto baada ya kuwa kwenye ndoa kipindi kirefu. Wengine wanaomba upenyo wa biashara, mume au mke wa ndoto zao. Wengine wanatamani wapate wafadhili wa kuwasomesha na kadhalika. Ili mradi matamanio yao kimaisha yatimie.

Hebu tuone wachache miongoni mwa hao, kwa yale wanayopitia. Dada mmoja alijitambulisha kwa jina la Grace, alinitumia ujumbe ufuatao. "Anti, naitwa Grace, nina umri wa miaka 34.

"Niliishi na mwanaume tukabahatika kupata mtoto mmoja ana umri miaka 12 sasa. Hivi sasa sipo na mwanaume huyo kwani tulishaachana miaka mitano iliyopita. Nahitaji mume sasa, nifanyaje? Nimesoma gazetini kisa cha Patty hajaoa, jamani mimi nahitaji mume wa ndoa naona umri unakwenda dada yangu!

Mpenzi msomaji, umemsikia dada huyu alivyo na shauku ya kupata mume wa ndoa. Huyo aliyezaa naye hakuwa amefunga ndoa naye. Wameishi miaka mitano na kupata mtoto bila ndoa. Analia kwa sababu ametambua kupoteza muda bila kutimiza ndoto yake ya kupata mume wa ndoa!

Baada ya kutafakari ujumbe wake ilibidi nimpigie simu dada huyu kujua zaidi kilichoendelea kati yake na mzazi mwenzake huyo. Akasema hivi;-Mwanaume huyo wakati bado tunaishi wote, alizaa na mwanamke mwingine mtoto mmoja.

Na baada ya kuachana na mimi, alioa mwanamke mwingine napo akazaa naye mtoto mmoja, naye pia wakaachana. Tena hivi sasa anaishi na mwanamke. Bwana huyu ni mfanyabiashara ndogondogo na mimi sina kazi. Ila natamani sana nipate mume wa ndoa", anamaliza kusema dada huyu.

Hapa zipo roho mbili zilizosimama kati ya bibie na baba mtoto wake huyo. Jamaa ana tatizo na roho ya mitala (kuoa wake wengi na kuacha). Ni mnyororo ambao unamwandama pasipo yeye kujua chanzo chake. Bibie naye anateswa na roho ya kucheleweshwa. Kuna kucheleweshwa kwa aina nyingi sana, mfano;- Kucheleweshwa kuzaa watoto, kucheleweshwa kuolewa, kucheleweshwa kufanikiwa kwenye biashara, kwenye kupandishwa cheo kazini na kadhalika.

Mungu alishasema na wanadamu kuhusu yote yale yanayotusibu kupitia neno lake. Akasema hivi;- "Kilichotarajiwa kikikawia kuja, moyo huugua, bali haja ya mtu ikipatikana, ni mti wa uzima(Mithali 13:12).

Watu wengi mioyo yao imeugua; hawana amani kwa sababu walichotarajia kwa miaka mingi kimechelewa. Pengine dada niliyemzungumzia hapo juu alitarajia mwanaume huyo angefunga ndoa naye lakini ameishia maumivu, wameachana bila ndoto kutimia.

Roho hii imechelewesha hatima za wengi sana. Hakika, wengi hawajafahamu uzito wa roho hii na hata wale wanaoifahamu wamekuwa wakipuuzia kuishughulikia. Watu wengi wanaona ni kawaida, kumbe ni shida! Mambo ambayo wangefanya kwa mwezi mmoja, wao wanafanya kwa miezi sita. Yale ambayo yangefanyika kwa mwaka mmoja, inawachukua miaka mitatu.

Watu wengine walipaswa kujenga nyumba zao kwa miaka miwili, cha ajabu sasa ni miaka mitano bado hawajamalizia. Tangu umefanya kazi sasa ni miaka 10 bado uko vile vile. Unapaswa kuolewa ukiwa na miaka 25, 26, 27 lakini sasa umri miaka 40 hujaolewa. Watu wa aina hii hawana raha kwa sababu walivyotarajia vimecheleweshwa.

Msomaji wangu, yamkini hapo ulipo hukupaswa kuwepo; tatizo umecheleweshwa! Kazi ya ibilisi ni kukucheleweshea baraka zako, hata kama ukipata hazitakuwa na umuhimu wowote. Kwa mfano, ukinunua gari una umri wa miaka 70, hilo gari halina faida kwako, maana umri hauruhusu kuendesha gari. Ungenunua gari hilo ukiwa na umri miaka 30 lingeleta faida kubwa zaidi.

Chanzo kikubwa cha kuchelewesha miujiza yako yetu ni shetani. Mungu anasema neno lake atakalolinena litatimizwa, wala halitakawilishwa. Neno halitakawilishwa ina maana kuwa "halitacheleweshwa". Mapenzi ya Mungu ni kutimiza ahadi zake upesi kwetu.

***Msomaji wangu, niishie hapa kwa leo. Je, una maoni, ushauri au kisa ungependa tujadili pamoja? Nitumie ujumbe kupitia 0715268581. Namba hii pia ipo WhatsAAP.***

# NAWAZA KWA SAUTI

Na Salome Kitomari



## Ushirikiano taasisi uhifadhi suluhisho ujangili mpya tembo

HIVI karibuni Shirika la Hifadhi za Taifa Tanzania (TANAPA), lilieleza kuwapo kwa aina mpya ya ujangili kwa kisingizio cha maini na mafuta ya tembo hutibu saratani na vidonda vya tumbo.

Aidha, imani hiyo impandikizwa kwa wananchi na watu wasio na nia njema kwa raslimali wanyama, kwa kuwa wananchi kwa njia mbalimbali wanaua wanyama hao na majangili wanachukua meno ya tembo.

Wananchi wameaminishwa kuwa maini ya tembo hutibu saratani ya ini na kizazi kwa wanawake, lakini vidonda vya tumbo na wengi wamejikuta wakiingia katika kuteketeza raslimali ya nchi kwa manufaa ya wanaochukua pembe.

Kutokana na tembo kutoka maeneo yaliyohifadhiwa kwa sababu mbalimbali kama kutafuata maji hasa wakati wa ukame au kusafiri kutoka hifadhi moja kwenda nyingine kupitia kwenye mapito yao ambayo hujulikana kama shoroba.

Kutokana na ongezeko la shughuli za kibinadamu, shoroba nyingi zimefunga kwa kuwa wananchi wamefungua mashamba, wamejenga makazi na shughuli zingine kiasi cha tembo wanapopita kwenye njia yao ya asili wanaishia kwenye migogoro na binadamu.

Utafiti unaeleza kwamba tembo ni mmnyama mwenye kumbukumbu kubwa kwa kuwa anauwezo wa kukumbuka na kupita njia aliyopita za wazazi wake miaka 100 iliyopita.

Wakati wanapita katika njia hiyo wamjikuta katika migogoro kwa kuwa binadamu hutegesha misumari na kuweka sumu kwenye maboga yanayoliwa na tembo ambao hufa na wananchi hushambulia mzoga kwa lengo la kupata maini na mafuta ya tembo.

TANAPA haijatoa takwimu za tembo waliouawa pamoja na maeneo ambako matukio hayo yametokea, lakini inaeleza kuwa ni mengi ambayo yanatishia uwepo wa raslimali hiyo.

Kwa takribani miaka miwili hakuna ujangili wa tembo kwa lengo la kupata kinachodaiwa ni dawa, na pia tangu TANAPA iwe na jeshi la uhifadhi au Jeshi Usu imesaidia mabadiliko ya mapambano dhidi ya ujangili kwa kuwa sasa zinatumika silaha za kivita na teknolojia kama ambavyo majambazi wanafanya.

TANAPA ni moja ya taasisi nyingi zinazohusika na uhifadhi zilizo chini ya Wizara ya Maliasili na Utalii, ambazo zina wajibu wa kulinda raslimali wanyama na misitu.

Nawaza kuwa bila ushirikiano wa dhati na pamoja kwa taasisi hizo, TANAPA haitaweza kupambana katika vita hivi vipya kwa kuwa yenyewe inahusika na usimamizi wa hifadhi za taifa 22, lakini wanyama wanapotoka nje ya hifadhi wanakuwa chini ya uangalizi wa taasisi nyingine.

Mathalani, TANAPA inasema eneo la ikolojia ya Selous ambako kuna Hifadhi ya Taifa ya Nyerere ujangili wa tembo ni mkubwa, kwa kuwa wanyama wanapotoka hifadhini kwenda kwenye Maeneo yaliyohifadhiwa na jamii (WMA) wanakutana na vikwazo kwa kuwa maeneo hayo yapo kisheria lakini hakuna utunzaji.

Ni lazima wanyama hao kutoka hifadhini humo kwenda Pori la Akiba Selous na baadaye Msumbiji ambako kote bado hakuna udhibiti wa kuwezesha usalama wao.

Inaelezwa kwa sasa kuna shughuli za kijamii zinaendelea katika ikolojia ya Nyasa Selous yenye ukubwa wa kilomita za mraba 160, kwa makundi makubwa ya wafugaji kuweka makazi huku wakivuna miti kwa kasi, pamoja na wakimbizi wa Msumbiji.

Bila ushiriki wa taasisi hizo tembo hawatabaki salama kwa kuwa sasa nguvu ya wananchi walioaminishwa kuwa watapano maradhi hayo ni kubwa na wanatumia mbinu nyingi za asili kuwapata wanyama hao.

> **"Ni muhimu taasisi hizi zikashirikiana vyema kutoa elimu kwa umma na kutoa ushahidi wa kisayansi kuwa hawawezi kupona maradhi hayo kwa kutumia maini au mafuta ya tembo.**

Ni muhimu taasisi hizi zikashirikiana vyema kutoa elimu kwa umma na kutoa ushahidi wa kisayansi kuwa hawawezi kupona maradhi hayo kwa kutumia maini au mafuta ya tembo.

Hakuna ubishi kuwa meno ya tembo soko lake kubwa ni nchi za Asia yaani Thailand, China na Vietnam ambazo bado hazijaonyesha utayari wa kuwa na sheria kali dhidi ya biashara hiyo.

Kichocheo kikubwa cha biashara hiyo ni imani na tamaduni zao kuwa viungo vya wanyama hao hutibu magonjwa mbalimbali kama homa, kupooza, huku wengine wakitaka kuwa na bidhaa zilizotengenezwa kutokana na pembe ya faru au meno ya tembo kama ufahari na heshima katika jamii, na wengi hutumia fedha nyingi ili kupata viungo hivyo.

Ushirikiano wa dhati chini ya utayari wa kisiasa uliopo nchini kwa sasa ndiyo msaada mkubwa katika kulinda raslimali hii muhimu inayoliingizia taifa fedha za kigeni.

***Tutafakari!***
***Mungu ibariki Tanzania.***

# HARUSI







## Tony na Grace

Antony Thompson na Grace Kiromo, waliungana kuwa mume na mke katika ndoa iliyofungwa Hoteli ya White Sands, jijini Dar es Salaam, Desemba 19, 2020 na baadaye sherehe kwenye garden ya St. Laurent, Mbezi Beach.







# MITINDO



UTATOKA HIVI

## Kipindi cha joto

KIPINDI cha hali ya joto kinaendelea, mwili wa binadamu unahitaji kupambana na hali hiyo ili kuhakikisha mtu anaendelea kufanya shughuli zake kama kawaida.

Katika kusaidia mwili kupambana na joto, unashauriwa kuvaa nguo nyepesi ambazo zitasaidia mwili kuwa na nafasi ya kupumua ili kupunguza mkandamizo wa hali ya hewa.

Kwa mujibu wa wataalamu wa masuala ya urembo wanasema mavazi aina ya fulana na zinazofanana na hizo ni nzuri kuvaliwa kipindi cha joto.

Lakini hapa nchini fulani zimekuwa maarufu si kutokana na kukabiliana na hali hiyo ya hewa, bali ni kutokana na urahisi wake wa kununua na kukabiliana na mazingira magumu.

Baadhi ya watu wanasema nguo za aina hiyo ni nyepesi, rahisi na pia haichagui aina ya nguo unayotaka kuvaa chini.

Hizi ni baadhi ya aina ya fulana ambazo unashauriwa kuwa nazo katika kipindi cha joto.

### FULANA ZA POLO

Fulana za Polo zimetengenezwa kwa kitambaa cha pamba, ina umbo jembamba ambalo hupenyesha hewa kwa urahisi.

Mara nyingi fulana ya aina hiyo inatengenezwa na kola pana eneo la shingoni, mikono yake mifupi kiasi na urefu wake unaishia kwenye eneo la mkanda.

Kutokana na mwonekano wake wa kuvutia, watu wengi hasa wanamichezo na watu maarufu wanapenda kuvaa wakiwa katika shughuli zao mbalimbali.

Fulana ya aina hii inapendeza sana kama mtu akifanya chaguo zuri la rangi, hasa zile ya kung'aa kama samawati, machungwa, njano, bluu na nyekundu.

Kitu cha kufurahisha, fulana za Polo hazichagui nguo chini kama suruali au kaptula.

### FULANA ZA MISTARI

Fulana zenye rangi ya mistari ni nzuri kuvaliwa katika hali ya hewa ya joto kama ilivyo sasa.

Fulana iliyotengenezwa ikiwa na kola au shingo fupi, zinafaa lakini hakikisha kitambaa chake kinatokana na pamba halisi.

Unashauri fulana ziwe za mikono mifupi na isiyobana sana mwili kwa wale wanaopenda usasa.

Unapotaka kununua fulana ya mistari hakikisha unafanya chaguo zuri la ubora, kwa sababu ukinunua yenye kitambaa imara itadumu kwa muda mrefu.

## UREMBO



### NYWELE ZAKO TU

# Ukizibana, ukiziachia utapendeza

NYWELE ni moja ya kionjo kinachochangia kumweka mwanamke katika mtazamo wa kuvutia.

Hata hivyo, baadhi ya wanawake hawatambui jambo hilo na badala yake wanaziachia bila matunzo kiasi ambacho humfanya mtu kupoteza mvuto na kuonekana kama kituko.

Urembo wa nywele unaonekana pale mtu anapozitunza vizuri, kuzisuka na hata kuzibana vizuri kulingana na mitindo anayoitaka katika muda husika.

Leo tuangalie namna kiungo hiki muhimu kinaweza kutumika kiubunifu ili kuboresha zaidi urembo wako.

Wapo baadhi husema eti nywele ndefu hazina mitindo mingi, pia kuna wanaofikiri nywele fupia hazinogeshwi kwa mitindo.

Nywele ndefu na zile fupi zinawezekana kuwekwa katika mitindo tofauti ambayo itakung'arisha na kuonekana mrembo.

**JINSI YA KUZITENGENEZA**

Kwa wenye nywele ndefu wanaweza kuziweka katika mitindo tofauti, ikiwamo kuzichana na kuzilaza nyuma, kuzibana kwa kutumia vibanio, au kuzifunga kwa kutumia mipira au vitambaa.

Pia wanaweza kuzichana na kuziachia 'Afro' huku akiwa amezipaka mafuta maalum ambayo yatang'arisha zaidi.

Kwa wale wenye nywele fupi, wana uwanja mpana wa kucheza na nywele zao, kwani wanaweza kuzichana kama kawaida au kuziweka dawa kidogo na kuzifanya zijikunje kama wimbi.

Kikubwa zaidi, kama ilivyo kwenye mavazi na urembo mwingine, unapaswa kuwa mbunifu wa namna kutafuta mitindo tofauti ya kuzibana, tusipende kukariri mmoja.

## MAPISHI

**Na Mary Geofrey**

# Njia za kupika mkate



ZIPO aina za mapishi mbalimbali ya mkate wa kawaida ambao unaweza kutumia maji au kuweka maziwa.

Mkate ni chakula ambacho huliwa wakati wa kufungua kinywa au chakula cha jioni.

Mkate hupikwa kwa kutumia unga wa ngano au wa muhogo. Chakula hichi kina wanga kwa kiasi kikubwa na hivyo husaidia kumpatia mlaji nguvu na joto mwilini.

**MAHITAJI**

Andaa unga wa ngano kilo moja (kwa familia yenye watu wengi kuanzia wanne, hamira gramu 50 na mayai manne.

Chumvi kijiko kimoja cha chai, sukari vijiko 2 vya chakula, maziwa fresh robo au 500 ml kama unauwezo basi tumia maji.

**NAMNA YA KUPIKA**

Hatua ya kwanza chekecha unga wa ngano kwenye chekeche ili kuondoa chenga kubwa pamoja na kuingiza hewa ndani ya chembe za unga.

Hatua ya pili weka hamira chumvi pamoja na sukari kisha koroga kwa mkono hadi uchanganyike vizuri kabisa. Hatua ya tatu koroga mayai yako 4 pembeni kwenye bakuli kisha mimina koroga yachanganyike ndipo uyamimine kwenye mchanganyiko wako, uyachanganye kwa mikono.

Hatua ya nne weka maziwa kwenye mchanganyiko wako na kisha ukande unga kwa vidole vyako hadi ulainike uwe kama wa kupikia chapati.

Hakikisha wakati unaukanda usizidishe maji, kwani kadiri unga unavyozidi kuumuka ndivyo unavyozidi kuwa laini.

Chukua chombo chako cha kuokea kipake mafuta ya samli kwa ndani, kisha kata unga kwa ukubwa unaotosha chombo chako na uutengeneze kwa umbo pembe nne.

Kama huna vyombo vya kupikia mkate waweza kutumia hata vya keki, ila usikate kwa maumbo ya mstatili.

Washa oveni yako kwa nyuzi joto dakika 120, kisha weka chombo chako chenye mikate na funga mlango.

Subiri dakika 30, mkate wako utakuwa umeshaiva na ili kujua kama umeiva vizuri, chukua kitu chenye ncha kali choma kwenye mkate na kama kikitoka kikavu hapo utakuwa tayari.

# MAISHA NI NYUMBA

**Na Elizabeth Zaya**

MPANGILIO

## Dondoo muhimu za kukipamba chumba cha kulala

**1:** Fahamu mtindo unaotaka kupamba meza yako ya pembeni. Ukijua itakusaidia kubuni mwonekano wa namna gani unataka uwepo katika meza yako.

**2:** Uwekaji wa picha ni moja ya njia ya kufanya chumba kionekane kizuri. Unaweza kuweka picha zinazokukumbusha mambo mazuri ya familia.

**3:** Weka trei ndogo kwa ajili ya kuweka vitu vidogo vidogo pembeni ya kitanda chako.

**4:** Unaweza kuongeza nakshi kwa kuweka maua pembeni ya kitanda ili kuongeza rangi. Maua kama ilivyo kwa taa ya mezani huongeza rangi na mvuto wa mwonekano.






# Namna ya kupanda mboga kwa makopo



NYUMBA ni sehemu ambayo inatumika watu kuishi, lakini inaweza kutumika kama sehemu ya kutengeneza bustani ya mboga.

Kama ambavyo nyumbani panaweza kutumika kwa ajili ya kutengeneza bustani ya maua. Vivyo hivyo inaweza kutumika kinyume chake.

Badala ya kuweka maua unaweza kuweka mbonga ambazo pamoja na kwamba inaweza kuleta mvuto kwenye nyumba, lakini ikaleta faida kutumika kama chakula.

Katika kufahamu zaidi namna ya kutengeneza bustani ya mboga, nilizungumza na Gerald Michael, mtaalam wa masuala ya bustani ambaye anabainisha namna ya kutengeneza bustani hiyo.

Anasema mojawapo ni kutumia makopo yale yale yanayotumika kupandia maua kandokando ya nyumba, kutumia gunia la sandarusi kubwa au ndoo.

Anasema katika vifaa hivyo vya unachanganya humo udongo, pumba za mpunga au mbolea ya samadi iliyooza vizuri.

"Udongo utasaidia kuwezesha mmea kusimama, pia kuupatia virutubisho, lakini pumba zitasaidia mizizi kupita kwa urahisi na kuweka mazingira mazuri ya hewa. Maji na mbolea ya samadi vitasaidia kutoa virutubisho kwa mmea na kuvichanganya kwa utaalamu.

Michael anasema makopo yanyotumika kupandia mboga ni lazima yatobolewe chini ili kuzuia maji kubaki kwa wingi na ndani yanatakiwa yawekwe pamba kwenye matundu yaliyotobolewa.

"Baada ya hapo unatakiwa kuweka udongo uliochanganywa vizuri kwenye makopo au ndoo, hapo utakuwa tayari umepanda mbegu zako ama mche wa mboga aina yoyote," anasema Maiko.

Kuhusu namna ya kuitunza anasema ni kuhakikisha unamwagilia angalau mara tu baada ya kupanda na kuendelea na kazi hiyo kutegemeana na aina ya mboga.


"Mboga kama sukuma wiki waweza vuna mara kwa mara, kazi yako ni kumwagilia tu. Unatakiwa kubadilisha udongo wako baada ya mavuno ili kuhakikisha mboga zako zina pata virutubisho ya kutosha," anasema Maiko.

Akielezea namna ya kutengeneza bustani hiyo kwa kutumia gunia, Maiko anasema yenyewe pia inaweza kutengenezwa katika sehemu yoyote ya eneo la nyumba. Anasema katika gunia pia unaweza kuchanganya udongo, pumba, mbolea iliyooza.

"Ziko hatua mbalimbali za utengenezaji wa mboga kwa kutumia gunia, toboa gunia lako na ondoa kitako ili kuweka uwazi juu na chini, weka mti au ubao katikati ya gunia ukiuchimbia ardhini, kisha weka gunia lako katikati ya mti au mbao hiyo na lijaze kokoto," anasema Maiko na kuongeza:

"Weka udongo uliochanganywa vizuri kwenye gunia lako na baada ya hapo hakikisha kokoto zinabaki zikizungukwa na udongo. Weka gunia juu ya kokoto zilizozungukwa na udongo kisha lijaze na kokoto, rudia kujaza udongo ukilizunguka hadi kimo cha gunia hilo. Endelea kufanya hivyo hadi pale gunia lako litakapokuwa limejaa."

# KATUNI


KATUNIKA KI'DOMOKRASIA
BY ABDUL KINGO - 2020
SMS - 0621 412 879
NNA KIMUHEMUHE CHA KUMWAGA 'MBWEMBWE' MANAKE SIJAWAHI KUKAA HUMU
JUKWAANI
DUH! UMENENEPA KAMA CHUPA YA SHAMPENI!
JAMAA ULIKUWA MFUPI KAMA MUKTASARI WA HABARI!
MWAKA UMEGEUKA UMEJIPANGAJE BAADA YA KUPIGWA CHINI JIMBONI?
BONDIA NUNDA HAOGOPI NGUMI ZA USO, NIME-JIPANGA KUWEKA "USO"
MANGI GANI MPAKA LEO UPO UPO HUJAKWENDA KUTAMBIKIWA!
USIKU NAPANDA NDEGE NAKWENDA ASUBUHI NARUDI KUFUNGUA DUKA
KWANI SIKU NYINGINE HAZIFAI KURUDI MAKWENU?
ZINAFAA LAKINI HAZINA 'VAIBU'
INJI HII WANANIKUBALI IPO SIKU UTASIKIA WAMENIPA IKULU 'NGOJA TU'
SINA HABARI NAISHI MAISHA YOTE NANENEPA BILA KUWA MJENGONI... KWANZA KUNA KELELE!
MBONA UNAJIHAMI! ...MIMI NAKUPA HERI YA MWAKA MPYA
*KINYUNYIZO CHA LEO...
...MWAKA MPYA UMEUONA......KIFUATACHO?

## HABARI KIMATAIFA

# Mtu mwingine mweusi auawa na polisi Marekani

**MENNEAPOLIS, Marekani**

POLISI wa Minneapolis nchini Marekani, wametoa video inayoonyesha mtu mweusi akiuawa kwa kupigwa risasi na polisi.

Kifo cha kijana huyo mweusi, Dolal Idd, kimekuwa cha kwanza cha aina hiyo, tangu mauaji ya George Floyd, yaliyoibua maandamano katika majimbo yote ya nchi hiyo.

Tukio hilo lilitokea Jumatano, baada ya Idd (23) akishukiwa katika tukio la kihalifu.

Walioshuhudia mauaji hayo walisema, Idd ndiye aliyeanza kuwafyatuli risasi polisi kabla ya walinda usalama hao kujibu mapigo.

Mei mwaka jana, mji wa Minneapolis ulishuhudia maandamano yaliyodumu kwa miezi kadhaa baada ya kifo cha Floyd aliyeuawa akiwa mikononi mwa polisi.

Maandamano hayo yalisambaa Marekani kote, huku kukiwa na madai ya ukatili yanayotekelezwa na polisi.

Floyd alifariki dunia baada ya ofisa wa polisi kupiga goti juu ya shingo yake kwa takriban dakika tisa na kusababisha kushindwa kupumua.

Video ya mauaji ya hivi sasa ya ufyatuaji wa risasi unaomhusisha ofisa wa polisi ilitolewa Alhamisi.

Katika video hiyo mpya, inaonyesha gari la polisi likizuia gari jingine jeupe katika kituo cha kuuza mafuta kusini mwa mji huo, eneo hilo mbali sana na alipouawa Floyd.

Maofisa wa polisi wanasikika wakipaza sauti wakisema "Simamisha gari lako, inua mikono yako juu, inua mikono juu!" Kabla ya kuanza kwa ufyatulianaji wa risasi kati ya kijana huyo na polisi.

Abiria wa kike aliyekuwa ndani ya gari la Idd, alipata majeraha, lakini hakuna polisi aliyejeruhiwa.

Mkuu wa Polisi wa Minneapolis, Medaria Arradondo, alisema bunduki moja ilipatikana kwenye eneo la tukio.

"Nilipotazama video ambayo kila mmoja anaitazama uhalisia wa mambo inaonekana aliyekuwa kwenye gari ndiye aliyeanza kufyatulia polisi risasi," alisema.

Watu kadhaa akiwamo baba yake Idd, Bayle Gelle, walikusanyika kwenye eneo la tukio siku iliyofuata, na kusababisha hofu ya kuanza tena kwa maandamano.

"Alikuwa ameketi tu ndani ya gari, na akaanza kufyatuliwa risasi bila sababu yoyote, alisema na kunukuliwa na shirika la habari la CBS News.

"Kwanini tumefika hapa? Kwasababu ya ubaguzi wa rangi. Ni mwanaume mweusi. Tunataka kujua kwanini kijana wangu alipigwa risasi na kuuawa." Alisema Gelle.

Meya wa mji huo, Jacob Frey, alisema amejitolea kuhakikisha anafahamu kwa undani kilichotokea na kuwa haki itatendeka.

"Tunajua maisha ya mtu yamekatizwa usiku huu na ule uaminifu kati ya jamii za watu weusi na maofisa wa polisi umezorota," alisema katika taarifa yake.

Aliongeza: "Kujenga tena uaminifu uliokuwapo kutategemea na uwazi tu."

**BBC**



Mtoto akiwa amebebwa na wafanyakazi kutoka meli ya uokoaji kutoka Hispania, baada ya kuopolewa baada ya boti aliyowabeba wahamiaji kuzidiwa na kuzama katika bahari ya Mediterranean, umbali wa maili 85 kaskazini mwa Libya juzi **(PICHA:AP)**

## Algeria yasaini katiba mpya kuwa sheria

RAIS wa Algeria, Rais Abdelmadjid Tebboune, amesaini katiba mpya ya nchi hiyo kuwa sheria.

Katiba hiyo iliidhinishwa mwezi Novemba baada ya raia wa nchi hiyo kupiga kura ya maoni na ilisainiwa na kiongozi hiyo baada ya kurudi nchini humo baada ya kuwapo Ujerumani kupatiwa matibabu ya COVID-19.

Rais Tebboune, alisema juzi kuwa alitia saini katiba hiyo ili kuleta mwanzo mpya kwa Algeria.

Kupitia katiba hiyo mpya, kiongozi huyo anajaribu kutuliza maandamano ya raia, maarufu kama vuguvugu la Hirak yanayoupinga uongozi wake.

Hata hivyo, katiba mpya iliungwa mkono na wapigakura wasiozidi asilimia 15 ya idadi wananchi nchini humo.

Raia wengi hawakujitokeza kwenda kupiga kura kutokana na janga la virusi vya corona pamoja na kuitikia wito wa Hirak wa kuisusia kura hiyo ya maoni.

**DW**

# Trump apata pigo la mwisho wabunge wake wamkataa

**WASHINGTON, Marekani**

RAIS wa Marekani, Donald Trump, amejikuta akifedheheka katika bunge la seneti la nchi hiyo, baada ya wabunge wa chama chake cha Republican, kuwaunga mkono Wademocratic, na kuishinda kura ya turufu ya rais kwa mara ya kwanza.

Maseneta hao waliupitisha mswada wa sera ya ulinzi ambao Trump, alikuwa ameupinga.

Kiongozi huyo amebakisha siku kadhaa kukaa Ikulu kabla ya nafasi yake kuchukuliwa na Rais mteulu Joe Biden.

Maseneta 81 waliunga mkono na 13 walipiga kura kukubali, na hivyo kupata theluthi mbili zinazohitajika ili kuishinda kura hiyo ya turufu.

Kulingana na sheria za Marekani, kura ya turufu ya rais ya kupinga mswada fulani inaweza kushindwa iwapo mswada unaojadiliwa unaungwa mkono na theluthi tatu ya wabunge katika mabunge yote.

Rais Trump alikuwa amekataa kuutia saini na kuufanya kuwa sheria mswada huo wa matumizi ya ulinzi wa dola milioni 750 kwa kuwa ulikuwa haujaondoa sheria kadhaa za kulinda mitandao ya kijamii.

Sababu nyingine ilikuwa mswada huo ulikuwa na kipengele kinachotoa nafasi ya kubadilishwa kwa majina ya kambi za jeshi, zilizokuwa zimepewa majina ya mejenerali yaliyokuwa yanaunga mkono utumwa.

Trump amekuwa haelewani na wabunge wa chama chake cha Republican, tangu apoteze nafasi yake katika uchaguzi wa mwezi Novemba baada ya wengi wao kutomuunga mkono.

**BBC**

SAFU

MAKALA

# Mafanikio yana njia nyingi



Na Magabilo Masambu

**Jambo baya linalofanyika katika familia zetu ni kurithisha chuki kwa watoto na hasa wanapofanikiwa. Nayakumbuka maneno ya Rais mstaafu Jakaya Mrisho Kikwete kwamba "siku zote usirithi adui wa mtu". Mama na baba mnakosana kwa sababu mnazozijua, mmojawapo anaanza kuwalisha watoto maneno dhidi ya mwenzake kwamba hakukusaidia.**

BABA popote ulipo, unikumbuke kwa kila ulifanyalo nakupenda. Uliondoka mjini miaka mingi iliyopita, uliahidi kurudi ututunze. Miaka mingi imepita sasa, bado hakuna ishara yako baba. Mama alikufa kwa mshtuko wa moyo miaka mingi iliyopita, aliposikia kwamba umeoa tena.

"Ni mimi pekee nimebaki katika familia hii, nikitangatanga katika mitaa ya Soweto.

Hakuna mahali pa kuita nyumbani kwangu. Nilijaribu kukutafuta miaka mingi iliyopita. Baba popote ulipo unikumbuke nakupenda."

Hii ni tafasiri isiyo rasmi ya maneno kutoka katika wimbo wa "Remember Me" ulioimbwa na mwanamuziki nguli wa reggae, Lucky Dube (sasa marehemu).

Historia ya maisha yake, inaonyesha kwamba alilelewa na bibi yake mzaa mama. Sababu kubwa ni baba yake kuondoka kwenda kutafuta maisha wakati hata Lucky Dube hajazaliwa. Kwa lugha nyepesi, tunaweza kusema kwamba baba alitelekeza familia.

Kutokana na ugumu wa maisha, mama yake pia alikuwa akienda huku na kule kutafuta fedha kwa kufanya vibarua kwa wazungu ili wajikimu. Kwa hiyo Luck akajikuta akilelewa na bibi yake. Haya ndiyo maisha yetu tulio wengi.

Kumekuwa na mjadala mkubwa sana siku hizi katika jamii zetu kuhusu fadhila za watoto kwa wazazi, hasa watoto waliofanikiwa kimaisha. Wako wanaosema kama baba au mama hajakutafutia maisha, anapozeeka na kuhitaji masaada wako, hastahili kwa sababu hakukusaidia! Wengine wanasema ni haki kupata msaada hata kama hawakushiriki kwa namna yoyote kukusaidia ukayapata mafanikio.

Pengine nitoe maoni yangu pia. Mipango ya Mungu si ya mwanadamu. Tumesikia wengi waliofanikiwa mara nyingi wakimshukuru Mungu kwa mafanikio, maana yake wamefanikiwa kwa mipango ya Mungu. Kwa hiyo pamoja na kuwalaumu wazazi wetu kwamba hawakutusaidia, lazima tufahamu pia wao hawapangi mafanikio yetu.

Inawezekana kutelekezwa kwako ilikuwa njia sahihi ya kuyafikia mafanikio uliyo nayo.

Nieleweke vizuri kwamba sipo hapa kutetea wazazi kutotimiza wajibu wao bali ukishafanikiwa si sahihi pia kuendelea kuwalaumu wazazi wako. Kazi moja waliyofanya ni kukuleta duniani.

Walikuwa na uwezo wa kukutoa ukiwa mimba, lakini angalau wamekuonyesha dunia.

Jambo baya linalofanyika katika familia zetu ni kurithisha chuki kwa watoto na hasa wanapofanikiwa. Nayakumbuka maneno ya Rais mstaafu Jakaya Mrisho Kikwete kwamba "siku zote usirithi adui wa mtu".

Mama na baba mnakosana kwa sababu mnazozijua, mmojawapo anaanza kuwalisha watoto maneno dhidi ya mwenzake kwamba hakukusaidia.

Pamoja na kwamba Lucky Dube alitelekezwa, bado anamtungia baba yake wimbo wa kumwambia anampenda sana na kwamba amemtafuta miaka mingi bila mafanikio. Duru zinaeleza kwamba wakati anauawa alikuwa kwenye harakati za kwenda Msumbiji kumtafuta baba yake, baada ya kupata taarifa kwamba yuko huko.

Ukweli tu nilio nao ni kwamba laana ya kumpa adhabu mzazi kwa kudhani kwamba hakukupa mafanikio uliyo nayo huwa inatembea. Zamu yako itafika utakuwa mzee utafanywa na watoto wako vivyo hivyo hata kama uliwasaidia katika mafanikio yao. Adhabu itabaki pale pale.

Mara nyingi ni vigumu sana kuyaelewa haya kama wazazi bado wako hai. Tumekuwa tukihangaika sana wakishafariki dunia kuweka picha zao kwenye kuta, kuweka katika mitandao ya kijamii na kwamba tunaumizwa sana, lakini tunashindwa kuwathamini wakiwa hai kwa sababu za kitoto sana kwamba hawakukusaidia. Wakati unazaliwa ulifahamu nani atafanikisha maisha yako?

Tusioyaamini haya tusome maandiko kuhusu kisa cha Yona kumezwa na samaki. Kwa ufupi Yona alitumwa na Mungu aende katika mji wa Ninawi ambako maovu yalikithiri sana, lakini akajiona mjanja eti amtoroke Mungu.

Akaenda kupanda meli kwenda Tarshishi. Akiwa kwenye meli mawimbi yakataka kuizamisha, mabaharia wakapiga kura ikaonekana yeye ndiye atolewe baada ya kukiri kwamba anamtoroka Mwenyezi Mungu!

Mabaharia wakamrusha baharini akamezwa na samaki na mwisho wa siku akafikishwa Ninawi na kuwahubiria watu waache maovu. Vinginevyo angewalaumu mabaharia kuwa walimtosa. Kwahiyo hata mafanikio yako yanaweza kuwa kama safari ya Yona. Inawezekana kabisa pengine wazazi wako unaowalaumu wangekusaidia katika yale wanayoona wao yanafaa usingefika ulipo.

Katika maisha, kuna watu wamezaliwa kutumika kama madaraja ya kuwavusha wengine na kazi yao ikikamilika huwa wanaondoka. Kwa hiyo unapoona mtu fulani amekusaidia usione kwamba ana maana sana kuliko wazazi wako.

Huyo ni daraja alikusudiwa kwako hamkukutana kwa bahati mbaya. Tunawasaidia sana marafiki ambao wakati mwingine hawajawahi kuwa sehemu ya mafanikio yetu bali wanatupenda kwa sababu ya mafanikio yenyewe.

Haikupunguzii chochote kumsaidia mzazi hata kama hakukusaidia, hivyo hukumu ya dhambi zake tumwachie Mungu.

Tukiwa mwanzoni kabisa mwa mwaka 2021, ni muhimu kufahamu kuwa hakuna mafanikio yenye historia nzuri yatakayokosa maumivu ndani yake.

Njia za kuyafikia mafanikio haziwezi kufanana kwa kila mtu. Kila mtu ana njia yake kama kilivyo kifo. Hakuna ajuae anakufa lini, wapi na kwa namna gani! Waliofanikiwa wengi wana historia ngumu na ndivyo maisha yalivyo.

**0689157789**
**magabilomjalifu@gmail.com**
**ARUSHA-TANZANIA**

BURUDANI ILIYOTIKISA ENZI HIZO

# Shoo ya 'Kubwa la Maadui' Mzee Ashanti



Na Adam Fungamwango

**Umaarufu wa mzee huyu ni kucheza kama adui kwenye filamu zake zote alizocheza wakati wa uhai wake, zaidi ya asilimia 90. Filamu ambayo akicheza kama mtu wa kawaida tu mwenye roho nzuri, mpenda watu, mwenye hekima na busara, watu wanakuwa hawaipendi. Ni kama wanaiona haina uhalisia.**

UNAPOZUNGUZIA filamu za Kihindi kama hujamtaja Mzee Amrish Puri, basi utakuwa hujakamilisha utamu wa picha hizo ambazo kwa watoto, vijana na wazee wa miaka ya mwanzoni mwa 1980 hadi mwanzoni wa miaka ya 1990 walikuwa wakizitazama sana kwenye kumbi mbalimbali za sinema kama Drive Inn, New Chox, Empire, Avalon na Cameo.

Alijulikana sana kwa majina mbalimbali ya kibabe. Wengine wakimwita 'bandidu' na kule Arusha walimfahamu kwa jina la 'Nyambisi', lakini India na sehemu zingine duniani wanamfahamu kwa jina la 'Mogambo'.

Jina aliitwa kutokana na kulitumia kwenye moja kati ya picha nyingi ambazo amecheza. Dar es Salaam na mikoa mingine nchini Tanzania, alijulikana kama Mzee Ashanti. Hili ndilo jina maarufu zaidi nchini na wakati mwingine ukitaja jina lingine, wengine wanakuwa hawamfahamu ni nani.

Jina la Ashanti alilipata kutokana na filamu moja aliyoicheza mwaka 1882, ilitwayo 'Ashanti'. Unyama alioufanya humo, watoto wa wakati huo waliamua kumpa jina la Mzee Ashanti.

Hata akionekana kwenye filamu zingine na hata akitumia jina lingine, wao wakimuona tu basi utasikia "adui kwenye picha hii ni Mzee Ashanti". Wengine wakamwita jina la 'Kubwa la Maadui."

Umaarufu wa mzee huyu ni kucheza kama adui kwenye filamu zake zote alizocheza wakati wa uhai wake, zaidi ya asilimia 90. Filamu ambayo akicheza kama mtu wa kawaida tu mwenye roho nzuri, mpenda watu, mwenye hekima na busara, watu wanakuwa hawaipendi. Ni kama wanaiona haina uhalisia.

Mzee Ashanti akicheza kama adui, kila anayeiangalia atataka atazame ubabe wake, ukatili wa kiwango cha juu, mwenye uwezo wa kumtesa na kumuua yoyote yule ambayo atahatarisha mamlaka yake, utajiri wake, au kitu chochote ambacho yeye anaamini yuko sahihi.

Hucheza kama mtu mwonevu, asiye na ubinadamu, mpenda makuu, katili, mvunja sheria, huku akiwaweka mfukoni baadhi ya maofisa wa polisi, na hata majaji wasio waaminifu.

Kutokana na kucheza kwa uhalisia mkubwa, alikuwa akipata mikataba mingi ya kucheza filamu nyingi tofauti.

Na hii inatokana na mashabiki wengi wa filamu za Kihindi kupenda kumuona na kupata uhalisia wa ukatili wa mzee huyo dhidi ya wananchi na masteringi ambao mara nyingi hupata tabu naye tabu mno, kabla ya kupata ushindi dakika za mwisho.

Ndiyo maana amecheza na wababe wote maarufu wa filamu za Kihindi kama kina Amitabh Bachchan, Sunny Deol na wengineo. Sidhani kama hajacheza na staa yeyote unayemfahamu wa miaka ya 1980 hadi 1990.

Inavyoonyesha soko la filamu la Kihindi lilitambua kuwa ili filamu ipendwe na kuuzwa sana, ni lazima Mzee Ashanti awepo. Tafuta 'steringi' yeyote yule, lakini kwenye nafasi ya adui lazima awepo mzee huyo ili mambo yaende kama yalivyopangwa.

Wale walioziona filamu za mzee Ashanti, wanajua shughuli yake isivyo ya kitoto. Kuna jamaa mmoja aliniambia kuwa kutokana na ukatili wa mzee Ashanti, basi adui yoyote kwenye picha la Kihindi basi alikuwa akimwita mzee Ashanti.

Mwingine akanidokeza moja kati ya ukatili wake kuwa kwenye filamu moja alikuwa anaoga maziwa, baada ya kuyaoga, wananchi wanamiminiwa kwenye bakuli na kulazimishwa kuyanywa.

Hizi ndizo baadhi ya shughuli zake kwenye filamu kiasi cha kuwaliza baadhi ya watazamaji kwenye roho ndogo, hasa kinadada na kinamama wanapokuwa akiangalia. Yaani hana shoo ndogo.

Shabiki mmoja wa filamu za Kihindi aliniambia kuwa alikuwa anamchukia kwa dhati kabisa mzee huyo kutokana na udhalimu wake, licha ya kwamba anafahamu kuwa alikuwa akiyafanya mbele ya kamera tu.

Habari kutoka nchini India zinasema kuwa nje ya filamu, mzee huyo alikuwa mtu wa watu sana na amesaidia watu wengi, ikiwamo maskini nchini India.

Alizaliwa Juni 22, 1932 na alifariki dunia Januari 12, 2005 nchini India kwa ugonjwa wa kansa.

Kutokana na kazi zake hizo, ataendelea kukumbukwa kizazi kwa kizazi, si nchini India tu, bali duniani kote kwa mashabiki wa filamu za Kihindi kuwa ndiye adui katili zaidi kuwahi kutokea kwenye filamu hizo mpaka sasa.

Waigizaji wengine ambao walikuwa wakicheza kama maadui nao wakatamba sana, ni Danny Denzongpa, maarufu kama Deni ambaye anachukua nafasi ya pili kwa ukatili kwenye nafasi ya kucheza kama adui baada ya Mzee Ashanti, Om Puri, Paresh Rawal, Vineet Kumar, Manoj Kumar, Surveen Chawla, Siddhant Kapoor, Nassorden Shah, Ronit Roy, Rahul Bhat, Girish Kulkarni, Prakash Ramchandani na wengineo.

HADITHI

# HADITHI

MILIO mitatu ya risasi ilisikika maeneo ya Keko Bora jijini Dar es Salaam. Sauti hizo za risasi ziliwafanya watu kutimua mbio na kutafuta chaka la kujificha. Kila mmoja alidhani ni majambazi waliovamia kwa ajili ya kupora pesa dukani au kwenye vibanda vya mawakala wa kampuni za simu. Haikuwa hivyo. Aliyedhaniwa kuwa ni jambazi alichofanya ni kumpora mwanamke mtoto mwenye umri wa mwaka mmoja tu na kuondoka naye akiwa kwenye gari aina ya Toyota IST. Huyu jamaa aliyefanya hivyo ni nani? Ni kwa nini amepora mtoto? Mtoto ni wa nani? Mwanamke aliyeporwa mtoto anamfahamu mporaji? Fuatilia kisa hiki kitamu, cha kusisimua na kuhuzunisha.

# Nina jambo langu-3

**Na Adam Fungamwango (0716 350534)**

Wakati anaongea maneno hayo, Jerry aligeuza kichwa chake na kwa mara ya kwanza alimkazia macho na kumtazama kwa makini msichana yule, akiushangaa uzuri wake.

Mwanamke alitabasamu, ndipo alipouona mwanya aliozidi kumchanganya.

"Naweza kukusogeza hadi Keko kwa sababu mimi nakwenda Chang'ombe."

"Sawa, haina neno."

Mazungumzo yaliendelea ndani ya gari. Alichogundua ni kwamba alikutana na msichana mchangamfu, tofauti kabisa na wengine ambao amewahi kukutana naye.

Pamoja na uzuri aliotunukiwa na Mwenyezi Mungu, bado hakujiona kuwa anapashwa kunata na kujiona.

Ni uzuri ambao kama wangepata baadhi ya wanawake wengine, basi Jerry angekuwa anapata kazi ya kuuliza tu maswali ni kujibiwa kwa kifupi. Tena wakati mwingine kwa nyodo na maringo.

"Unaitwa nani bibie?"

"Naitwa Neema."

"Jina zuri."

"Ni kweli zuri, neema siku zote ni nzuri tu."

"Mimi naitwa Jerry."

"Okay, nashukuru kukufahamu kaka."

Moyoni mwa Jerry kulikuwa kuna kitu kinafukuta. Alishampenda msichana yule. Tatizo lilikuwa ni kumwambia tu.

Kumwambia anaweza, lakini mapema kiasi kile, itaonekana anamuona ni mmoja wa wale wanawake wasiojiheshimu na anaweza kukataa. Pamoja na kiu yake, hakutaka iwe mapema kiasi kile. Akatengeneza mazingira ya kuomba namba. Akaipata.

******************************


Siku tatu zilipita. Ilikuwa kama vile alitaka kumsahau. Haikuwa hivyo. Ilikuwa mchana, akipata chakula maeneo ya Mwenge jijini Dar es Salaam, barabara ya Sam Nujoma karibu kabisa na Mawasiliano na ndiko karibu na ofisi yake alimpigia simu.

Ilipokewa na sauti laini ya "Haloo"

"Niambie bibie za siku mbili tatu."

"Nzuri tu, za kunisusa?"

"Sijakususa bibie, mambo tu ya mjini hapa, yanaingiliana."




**Kwa mara nyingine tena, Jerry alikutana na uzuri wa msichana Neema. Neema Neema kweli. Alivaa gauni la bluu lililombana, lakini likiacha nusu ya miguu yake kuanzia kwenye magoti kushuka chini ikiwa wazi.**

"Hakuna neno, usijali."

"Sasa kama leo una nafasi tuonane."

"Wapi?"

"We sema tu nije nikuchukue wapi?"

"Mimi nafanya kazi Sinza, nitatoka hapa saa 10 jioni, utanifuate Bamaga."

Kwa mara nyingine tena, Jerry alikutana na uzuri wa msichana Neema.

Neema Neema kweli. Alivaa gauni la bluu lililombana, lakini likiacha nusu ya miguu yake kuanzia kwenye magoti kushuka chini ikiwa wazi.

Kwake Jerry ni kama alikuwa ameongezeka uzuri zaidi ya yule aliyemuona siku ile Makumbusho. Maeneo hayo kulikuwa na hoteli nzuri tu pembeni kidogo ya kituo cha mafuta.

"Twende kwanza tukale, halafu ndiyo twende nyumbani." Jerry alimwambia Neema.

Hapana shaka, walipoingia walipendeza kiasi kwamba kama ukisema kuwa hawa si mtu na mpenzi wake, basi ungeweza kupigwa mawe kwa madai ya uongo. Walikaribishwa na mhudumu ambaye aliwauliza mahitaji yao. Jerry alielekeza mkono kwa Neema ili achague anachokitaka.

"Chips kuku na soda baridi." Aliagiza.

"Mimi niletee maji, ugali na nyama ya kuchoma." Hicho ndicho alichoagiza Jerry. Chips na kuku zilitelemka taratibu kwenye kinywa cha Neema, huku ugali na nyama ya kuchoma ukiteketea kwenye tumbo la Jerry.

Ilipita dakika saba hivi kila mtu akila, wakiwa na utulivu wa muda, baada ya muda mrefu wa mazungumzo.

"Naomba nikwambie kitu Neema." Sauti ya Jerry ilisikika ikiwa kama ina mikwaruzo.

"Kitu gani?"

"Eeeh, Neema wewe ni mwanamke mrembo. Na tangu nilivyokuona siku ile kule Makumbusho na nikakupa lifti hadi Keko, nimetokea kuvutiwa na wewe."

Neema alitabasamu, akainamisha kichwa kwenye meza. Akainua tena na kumtazama Jerry kwa aibu.

"Enhee." Alisema kama vile anataka kucheka, kana kwamba anajua kile ambacho anataka kukisema.

"Naomba uwe mpenzi wangu." Ni neno ambalo baada ya kulitamka, Jerry alishusha pumzi, kana kwamba lilikuwa na uzito wa tani elfu moja.

Kwa nusu dakika hivi, Neema hakujibu kitu. Halafu naye anashusha pumzi na kuonekana kama alilipokea neno lile kutoka kinywani mwa Jerry lililokuwa na uzito mkubwa na yeye akalibeba kwa uzito huo huo.

"Pole sana Jerry. Tena pole sana." Jibu lile lilimshtua mno.

"Mimi nimeolewa miaka mitatu iliyopita. Mimi hapa ni mke wa mtu. Kama tungeonana kabla ya hapo, wala isingekuwa shida. Lakini kwa sasa nina mume na nimezaa naye mtoto mmoja ana mwaka moja sasa."

******************************

Hayo ni mawazo ya Jerry aliyokuwa akiyakumbuka kutokea kiasi cha miezi minne iliyopita.

Alichokiona ndicho kilichomkumbusha yote hayo. Baada ya kupiga picha gari ambalo aliyemteka mtoto wa Neema aliondoka nalo, aliamua kushuka chini kwa kutumia ngazi kwa kasi.

Alitaka kwenda kuchukua gari lake alilopaki, lakini akabadili mawazo ghafla. Alijua mbele ya safari anaweza kukwama kutokana na foleni kubwa kwenya makutano ya barabara ya Kawawa na Nyerere maeneo ya VETA.

Akataka kukimbilia kwenye kituo cha bodaboda, lakini kabla hajafika, kuna bodaboda moja ilikuwa ikitokea Chang'ombe na kukata kona kuelekea Uwanja wa Benjamin Mkapa, akaipungia mkono. Mwendesha bodaboda akageuza.

"Unaweza kuendesha kwa mwendo wa kupaa?"

"Hilo tu mwanangu, bora useme lingine." Alijibu kijana huyo kwa kujiamini huku akitabasamu. Wakati akijibu, tayari Jerry alikuwa ameshadanda kwenye kiti cha abiria.

"Nataka ukimbie haraka, kuna gari moja nalifuata, nitakuonyesha kama tutafanikiwa kuliona."

"Gari la aina gani?" Aliuliza.

"Ni hivi, wewe endesha, mimi nitakapoliona nitakwambia kama ni lile, halafu baada ya hapo utafuata maelekezo yangu."

"Malipo?"

"Usijali, nitakulipa utakachohitaji." Jerry alimjibu na wakati huo huo, bodaboda ikichanja mbuga kwenda maeneo ya Keko anapouza vitanda, viti, meza na vitu vingine vya ndani.

**INAENDELEA JUMAPILI**


Fik Famei


KiDi



## ZUCHU HAKAMATIKI

# UREMBO, KAZI ZAKE MOTO AFRIKA

MWAKA 2021 unatarajiwa kuwa wa mafanikio kwa wasanii wa muziki wa Afrika, baada ya 2020 kuwa wa neema kwa wanamuziki wengi.

Kulingana na Shirika la Utangazaji la Uingereza (BBC) mwaka 2020, ulimwendea vyema mwanamuziki aliyechipukia kwa kasi, Zuchu, na kumfanya aongoze nyimbo zake kutazamwa na watu wengi.

Zuchu ambaye ni mtoto wa mwimbaji wa taarabu nchini, Khadija Kopa, ameweza kuwavutia watazamaji wengi katika mtandao wa You Tube, kutokana na nyimbo zake kali na zinazoweza kumtoa nyoka pangoni.

Akitumia lugha ya Kiswahili na Kiingereza, ana sifa za kuwa mwamuziki nyota wa Bongo Fleva.

Mwaka uliopita msanii huyu alizindua Albam yake iliyoitwa I AM Zuchu, na kumpa maadili mengi yanayomwingizia fedha nyingi.

Kwa mujibu wa programu ya kucheza muziki ya Boomplay, albamu yake hiyo ndio iliyochezwa sana mwaka 2020 na video za muziki wake zimefanikiwa kuvutia mamilioni ya mashabiki katika mtandao wa You Tube.

### Fik Fameica (Uganda)

Fik Fameica, anajulikana kama Fresh Boy, ni mmoja wa wanamuziki wa aina ya Rap anayevutia wengi Afrika Mashariki.

Mara ya kwanza mwanamuziki huyo alitoka na ngoma yake 2017 iliyoitwa 'Kutama' ambayo ilipendwa na mashabiki wengi.

Kijana huyo hapigi muziki kama ule unaochezwa na wasanii wengine nchini Uganda, yeye muziki wake unafanana na rege.

Fik Fameica tayari amefanya kolabo na wanamuziki maarufu Afrika, akiwamo Patoranking, Vanessa Mdee na Joeboy.

### Gaz Mawete (DRC)

Gaz Mawete, alianza muziki 2018 kwa kutumia aina ya muziki ya Olingi Nini, na alipanda kwa kasi na kuwa maarufu duniani kwa kupiga muziki wa Kifaransa.

Mcheza densi huyo wa Dk. Congo, ambaye alipata umaarufu nchini kwake baada ya kushiriki katika mashindano ya kusaka vipaji, amefanya kolabo na wakali wa muziki wa dansi kama fally Ipupa ambaye alionekana katika wimbo wa C'est Rate.

Mawete pia alishiriki katika albamu ya Dadju Poison au Antidote.

### Kabza De Small (Africa Kusini)

Kabza De Small, amewavutia wapenzi wa muziki tangu alipoanza kutoa nyimbo zake mwaka 2016.

Dj huyo na mtayarishaji wa muziki, amepewa jina la utani la 'Mfalme wa Amapiano', amekuwa na aina moja ya muziki nchini Afrika Kusini.

Muziki wake una nguvu na kuvutia. Kabza De Small amekuwa mzuri katika sauti ambayo imeanza kusambaa katika nchi zingine za Kiafrika.

Ushawishi wake unaweza kusikika katika nyimbo zilizorekodiwa na alijulikana sana baada ya kuchaguliwa katika tuzo za MTV.

### KiDi (Ghana)

Kidi, ni sehemu ya kizazi kipya cha wasanii wa Ghana, ambaye alipata mafanikio wakati kibao chake cha Sugar kiliposhinda tuzo za muziki nchini humo.

Muziki wa msanii huyu umechanganyika na midundo ya Afrika na unamfanya kuwa msanii ambaye muziki wake unaweza kusikilizwa na watu walio nje ya mpaka wa Ghana.

Mnamo mwaka wa 2020, wimbo wa KiDi Say Cheese, kutoka kwa albamu yake Blue, ulimpatia umaarufu wa kimataifa baada ya msanii wa Marekani Teddy Riley kushirikiana naye kwenye remix.

# Coutinho nje ya dimba hadi Aprili

**BARCELONA,** Hispania

PHILIPPE Coutinho jana Jumamosi alitarajiwa kufanyiwa upasuaji wa goti na anatarajiwa kuwa nje kwa kipindi kirefu, kwa mujibu wa taarifa kutoka klabu ya Barcelona.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Brazil aliingia akitokea benchi dakika ya 66 Jumanne, wakati Barcelona walipotoka sare ya bao 1-1 na Eibar katika dimba la Camp Nou kwenye mchezo wa Ligi Kuu Hispania.

Ijumaa, Barca ilithibitisha kwamba mchezaji huyo atafanyiwa operesheni ya goti lake la kushoto, baada ya hapo ratiba ya kurudi kwake uwanjani itatolewa. Taarifa ya klabu ilisomeka: "Philippe Coutinho atafanyiwa upasuaji Jumamosi hii kwa jeraha la goti la kushoto na Dk. Joan Carles Monllau chini ya usimamizi wa huduma za matibabu za klabu.

"Mara tu upasuaji utakapokamilika, habari zaidi itatolewa kwa kina kuhusu muda unaotarajiwa wa kupona."

Vyombo kadhaa vya habari vya Hispania vimeripoti kwamba mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28 anaweza kuwa nje ya uwanja kwa kipindi kirefu, labda hadi Aprili.

Kukosekana kwa muda mrefu kwa mchezaji huyo litakuwa ni pigo jingine kwa bosi wa Barca, Ronald Koeman, ambaye tayari hana Ansu Fati, Sergi Roberto na Gerard Pique kutokana na majeraha. Coutinho amecheza mechi 14 kwa Barcelona msimu huu kwenye mashindano yote, akifunga mabao matatu na kutoa asisti mbili.

Alitumia msimu uliopita kwa mkopo huko Bayern Munich, akiisaidia klabu ya Ujerumani kupata mataji matatu ambayo ni pamoja na kushinda Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Uvumi ulikuwa umesambaa kwamba anaweza kuondoka klabuni hapo kwenye dirisha la usajili la Januari hii, lakini kikwazo hiki cha hivi karibuni kinaonekana kuhakikisha kuwa na Barca kwa msimu 2020-21.




# UNITED HAWANA PRESHA NA SANCHO




**MANCHESTER,** England

KLABU ya Manchester United haina presha na usajili wa Jadon Sancho kutoka Borusia Dortmund mwaka huu, kwa mujibu wa ESPN.

Habari ya Sancho kutimkia United iliteka dirisha la usajili wa kipindi cha majira ya joto kilichopita, lakini mwisho wa siku usajili haukufanyika.

Na sasa kwa mujibu wa ripoti kutoka kwa mabosi wa United, Sancho anaweza kutua pale Old Trafford kipindi kijacho cha majira ya joto.

Tangu usajili wa Sancho uliposhindikana, kiwango cha mchezaji huyo msimu huu kimeonyesha ni kiasi gani ameathirika kisaikolojia kwa kushindwa kujiunga na miamba hiyo ya Old Trafford.

Hadi sasa kwenye Ligi Kuu Ujerumani, Bundesliga, Sancho hajafunga goli lolote na hayupo kwenye kiwango alichokuwa nacho msimu uliopita.

Licha ya kiwango duni msimu huu, United bado wanaamini wanaweza kumsajili Sancho mwaka huu tena kwa kiasi cha chini ya pauni milioni 100.

Dortmund waligoma kumwachia Sancho kwa dau hilo wakishinikiza kutaka pauni milioni 120, ambayo uongozi wa klabu hiyo haukuwa tayari kutoa kiasi hicho hasa wakati huu ambao mlipuko wa virusi vya corona ukiwa umeathiri sana uchumi kwa sehemu kubwa.

# *Pioli kuipeleka Milan Ligi Mabingwa Ulaya*

**MILAN,** Italia

STEFANO Pioli amesisitiza AC Milan wanalenga kurudi kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya na amesema pia Simon Kjaer na Zlatan Ibrahimovic "wameleta mabadiliko" makubwa klabuni hapo.

Milan walitawala soka la Italia mwaka 2020 na kumaliza mwaka wakiwa vinara wa msimamo wa ligi, wakiwa juu kwa alama moja dhidi ya wapinzani wao Inter Milan. Lakini hata kama wanaongoza mbio za taji la Serie A, Pioli amesisitiza kuwa lengo lao kuu ni kuirejesha Milan kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya.

"Tutafanya bidii ili kujiboresha. Naam, turudi kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya. Klabu haijahitaji chochote, hawataki kutupa shinikizo kwa sasa."

"Sisi sote tunatambua lazima tufanye kila tunaloweza kuirudisha Milan mahali pake, kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya."

Huenda huu ukawa ni wakati haswa wao, baada ya kufanya vyema kipindi hiki huku wakionekana kuwa na mipango ya kutoboa zaidi katika msimu.



# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# SOLSKJAER: MBIO ZA UBINGWA EPL NGUMU

Aeleza kikosi chake kinaimarika huku akiweka wazi msimu huu kutakuwa na matokeo...

**MANCHESTER,** England

KOCHA Ole Gunnar Solskjaer anaamini mbio za ubingwa wa Ligi Kuu England msimu huu zitakuwa "ngumu sana", wakati Manchester United ikijivuta kileleni mwa msimamo kwa kuwa pointi sawa na Liverpool.

United iliichapa Aston Villa mabao 2-1 pale kwenye dimba la Old Trafford, Ijumaa usiku, ikibakia nafasi ya pili nyuma ya bingwa mtetezi Liverpool, lakini wamelingana pointi na wanatofautiana mabao.

Ulikuwa ni ushindi wa 10 mfululizo kwenye Ligi Kuu bila kufungwa kwa kikosi hicho cha Solskjaer ambapo walinufaika na suluhu ya Liverpool dhidi ya Newcastle United, Jumatano.

**Liverpool inaweza kujikita zaidi kileleni kama ikiwafunga Southampton katika mchezo wa kesho Jumatatu, huku United ikiwa na mchezo mmoja mkononi dhidi ya Burnley, lakini Solskjaer anatarajia mbio za ubingwa huo kuwa ngumu sana.**

"Tumeimarika, tuko bora zaidi," amesema kocha huyo akiiambia Sky Sports. "Ligi na msimu utakuwa mgumu sana.

"Kutakuwa na mechi tofauti na ngumu, matokeo ya ajabu, tutaendelea kujituma na kuimarisha timu.

"Tangu mwishoni mwa msimu uliopita, tumekuwa na mwendelezo mzuri wa matokeo mazuri. "Kila wakati unashinda mchezo, unachukua hatua moja mbele. Ni pointi tatu kwa ujumla, unatakiwa kuzijumulisha.

"Mchezo wa kwanza ni muhimu kama mchezo wa mwisho wa msimu uliopita - inahesabiwa vile vile."

Baada ya Anthony Martial kufunga bao la kuongoza, likasawazishwa na Bertrand Traore, na Bruno Fernandes akaifungia United bao la ushindi kwa mkwaju wa penalti dhidi ya Villa, ambao hawajashinda mechi 16 za ligi walizokutana na United.

## ZISIKUPITE

### SANCHO KWENYE RADA

MANCHESTER United wanaamini wanaweza kumsajili winga wa Timu ya Taifa ya England, 20, Jadon Sancho kutoka Borussia Dortmund kwa chini ya pauni milioni 100 mwaka huu. ***(90 Min)***

### DELE, ERIKSEN WATAKIWA

KOCHA mpya wa Paris St-Germain, Mauricio Pochettino amehusishwa na wachezaji wake wawili wa zamani kule Tottenham Hotspur, Dele Alli, 24, na Christian Eriksen mwenye miaka 28, ambaye kwa sasa anacheza Inter Milan. ***(AS)***

### SHAQIRI KUBAKI LIVERPOOL

LIVERPOOL wamebadili msimamo wao dhidi ya winga wa kimataifa wa uswisi, Xherdan Shaqiri, 29, na sasa hawatamruhusu kuondoka mwezi huu. ***(Liverpool Echo)***

### ARSENAL YAMTAKA CHRISTIE

ARSENAL imeingia kwenye mbio moja na timu kadhaa za Ligi Kuu England kumwania kiungo wa Celtic ya Scotland, Ryan Christie (25), na wanamatumaini mlinzi wao wa kushoto, Kieran Tierney mwenye miaka 23, anaweza kumshawishi raia mwenzake huyo kutua pale katika dimba la Emirates. ***(90 Min)***

### ARTETA AMPOTEZA OZIL

KOCHA wa Arsenal, Mikel Arteta hana uhakika kama kiungo wa Ujerumani, Mesut Ozil atarudi kwenye kikosi. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 32 hajaichezea Arsenal msimu huu. ***(Sky Sports)***

### MOURINHO NA USAJILI

KOCHA Jose Mourinho amesema "utakuwa mshangao mkubwa" kama Tottenham wataingia sokoni Januari hii na amesisitiza hatamwomba mwenyekiti, Daniel Levy kuongeza wachezaji. ***(Standard)***

### ZAHA NJIA PANDA

KOCHA wa Crystal Palace, Roy Hodgson amesema hajui chochote kuhusu majaliwa ya Wilfried Zaha, huku AC Milan na Paris St-Germain zikiwa ni timu zinazohusishwa na kuwania kumsajili fowadi huyo wa kimataifa wa Ivory Coast mwenye umri wa miaka 28. ***(Mail)***

### BRAAF ANUKIA DORTMUND

KLABU ya Borussia Dortmund inawania kumsajili winga wa Manchester City, Jayden Braaf ambaye ana umri wa miaka 18 na ni raia wa Uholanzi. ***(Bild, via Mail)***

### ZIDANE: HAWAONDOKI

KOCHA wa Real Madrid, Zinedine Zidane amekanusha madai kwamba, kiungo wa kimataifa wa Croatia, Luka Modric mwenye umri wa miaka 35, mlinzi wa Hispania, Sergio Ramos mwenye miaka 34, na Lucas Vazquez mwenye miaka 29, wataondoka klabuni hapo. ***(Team Talk)***

### HOLDING, ARSENAL SAFI

MLINZI wa Arsenal, Rob Holding mwenye umri wa miaka 25, anakaribia kufikia makubaliano ya kusaini mkataba wa muda mrefu, na kumaliza uvumi wa kutaka kuondoka. ***(Telegraph)***

HABARI MICHEZO

## Azam yapitia dk 540 chungu

**Na Adam Fungamwango**

HATIMAYE kikosi cha Azam kimeondoa gundu la kutopata ushindi katika mechi sita mfululizo za Ligi Kuu Bara, baada ya juzi Alhamisi kupata ushindi wa bao 1-0 kwenye Uwanja wa Ushirika Mjini Moshi dhidi ya wenyeji Polisi Tanzania.

Azam iliwatia hofu mashabiki wake baada ya kucheza mechi sita mfululizo bila kupata ushindi na kuzua maswali mengi kwa wadau wengi wa soka kutokana na uwezekaji na matokeo inayoyapata.

Kocha Msaidizi wa timu hiyo, Vivier Bahati, alisema ushindi walioupata katika mechi ya kwanza ya mzunguko wa pili ni ishara kuwa mambo yamekaa sawa na sasa hali itarejea kama kawaida.

"Tulianza ligi msimu huu na Polisi Tanzania tulishinda bao 1-0 nyumbani, sasa tumeshinda tena, ni jambo zuri. Mungu ametuona, ametupa pointi tatu, naamini sasa mambo yatakuwa mazuri," alisema kocha huyo.

Bao lililofungwa dakika tatu kabla ya mechi hiyo kumalizika na mchezaji asiye na jina kubwa, Ismail Aziz Kaden, liliipa Azam ushindi wa kwanza tangu Novemba 5, mwaka jana, ilipoifunga Dodoma Jiji FC mabao 3-0 kwenye Uwanja wa Azam Complex jijini Dar es Salaam.

Baada ya hapo ilicheza mechi sita bila kupata ushindi, ikifungwa mechi mbili na kutoka sare nne.

## Amri atangazwa kuinoa Mwadui

**Na Saada Akida**

UONGOZI wa Mwadui FC umeingia mkataba wa miezi sita na aliyekuwa Kocha wa Mbeya City, Amri Saidi kwa ajili ya kuinusuru timu hiyo inayoburuza mkia katika msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara, imefahamika.

Amri, beki wa zamani wa mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara amechukua mikoba iliyoachwa na Khalid Adam ambaye alitimuliwa klabuni hapo hivi karibuni.

Akizungumza na gazeti hili jana, Mwenyekiti wa Mwadui FC, Nurdin Selemani, alisema uongozi wa klabu hiyo ulifikia makubaliano na Amri jana asubuhi, hivyo kwa sasa rasmi ni kocha wao.

Selemani alisema baada ya kusaini mkataba huo wa miezi sita, wamekubaliana kuanza kufanya mchakato wa usajili kwa kuongeza nguvu kwenye idara ambazo zina upungufu ndani ya kikosi hicho.

"Hatukufanya usajili, tulisubiri tumalizane na Kocha Mkuu Amri Said, halafu tumkabidhi ripoti ambayo tulikabidhiwa na mwalimu aliyeondoka kuhusu nafasi za usajili kwa ajili ya kuimarisha kikosi chetu," alisema kiongozi huyo.

Alitaja nafasi ambazo zinahitaji kuimarishwa ni ya ushambuliaji, ulinzi na mchakato wa kuwapata wachezaji hapo utaanza mapema kabla ya dirisha la usajili halijafungwa.

# MWAKALEBELA AFUNGUKA KINACHOING'ARISHA YANGA

**Na Shufaa Lyimo**

WAKATI timu yao ikiendelea kushikilia rekodi ya kutopoteza mechi yoyote msimu huu, Uongozi wa Yanga umesema kikosi chao kitaendelea kucheza soka la ushindani mpaka lengo lao la kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu litimie.

Akizungumza na gazeti hili jana, Makamu Mwenyekiti wa Yanga, Frederick Mwakalebela, alisema wamejipanga kuona timu yao inazidi kuimarika ili kuendeleza kasi ya ushindi waliyokuwa nayo kwenye ligi hiyo inayotoa tiketi ya kushiriki mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Mwakalebela alisema uongozi pia umejipanga kusajili wachezaji wenye viwango vya juu ambao wataisaidia Yanga kupata mafanikio wanayoyatarajia katika msimu huu.

**"Tunashukuru mchezo wetu wa kwanza wa mzunguko wa pili ulimalizika salama, tuna malengo ya kuutwaa ubingwa msimu huu, hivyo ni lazima tuendelee kuonyesha soka la ushindani katika kila mechi," alisema Mwakalebela.**

Kiongozi huyo alisema pia umoja waliokuwa nao viongozi, wachezaji, wanachama na mashabiki umesaidia kuzalisha matokeo mazuri katika michezo yote waliyoicheza.

"Siri ya mafanikio ni umoja ambao tunao sisi na wachezaji wetu, mikakati yetu ni kuwa mabingwa tu, hakuna jambo lingine," Mwakalebela alisema.

Aliongeza tayari kikosi chao kimesharudi jijini Dar es Salaam na kimeanza mazoezi kwa ajili ya kushiriki mashindano ya Kombe la Mapinduzi ambayo yatafanyika Zanzibar kuanzia Jumanne Januari 5, mwaka huu.

Alisema pia ujio wa Kocha, Cedric Kaze umechangia kuleta mafanikio ndani ya klabu hiyo jambo ambalo linaonekana na kila Mwana-Yanga.

Katika mashindano ya Kombe la Mapinduzi, Yanga imepangwa kuanza kampeni hiyo kwa kuwavaa Jamhuri siku ya Jumanne na Januari 8, mwaka huu itakamilisha hatua ya makundi kwa kuwakabili Namungo huku Januari 6, mwaka huu Simba ikikutana na Chipukizi wakati Januari 9, mwaka huu itavaana na Mtibwa Sugar.




Mkurugenzi wa Utawala na Udhibiti SportPesa, Tarimba Abbas, akimkabidhi mfano wa hundi ya Sh. 23,300,000 Mwenyekiti wa Namungo FC, Hassani Zidadu, kama mchango wa kukamilisha safari yao kuelekea mechi ya Sudan dhidi ya Al Hilal. Namungo FC wamefanikiwa kupita katika hatua nyingine kwenye Kombe la Shirikisho Afrika. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# *Spotpesa yatoa udhamini wa Sh.mil 23.3*

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya Michezo ya Burudani ya SportPesa imeipa udhamini wa Sh. milioni 23.3 klabu ya Namungo FC kwa ajili ya kuiwezesha timu hiyo katika Kombe la Shirikisho Afrika.

Hiyo ni katika kuelekea mchezo wao dhidi ya Al Hilal ya nchini Sudan utakaopigwa Januari 6, mwaka huu wa marudiano.

Akizungumza na waandishi wa habari, Mkurugenzi Uendeshaji wa SportPesa, Tarimba Abbas, alisema kuwa udhamini huo walioutoa maalum kwa ajili ya mchezo dhidi ya Hilal.

Tarimba alisema kuwa fedha hizo zitaiwezesha timu hiyo, kununua tiketi na matumizi mengine katika kuelekea mchezo huo mgumu ambao anaamini Namungo itapata ushindi.

"Katika kuthamini michezo SportPesa tumewapa udhamini Namungo kwa ajili ya kuwezesha baadhi ya vitu katika kuelekea mchezo huo na kati ya hivyo ni tiketi za ndege kwa wachezaji na viongozi.

"Pesa hiyo ya Sh. milioni 23.3 ni ndogo, lakini tunaamini kuwa itaisaidia kwa kiwango kikubwa Namungo katika kuelekea mchezo huo.

"Hatuna wasiwasi na Namungo katika kuelekea mchezo huo, tunaamini watapata matokeo mazuri na kusonga mbele katika mashindano hayo makubwa Afrika.

"Lengo la SportPesa kutoa udhamini huo kwa Namungo ni kuona michezo inapiga hatua, hivyo SportPesa itaendelea kutoa udhamini kama ilivyokuwa kwa klabu za Simba na Yanga," alisema Tarimba.

Akipokea hundi hiyo, Mwenyekiti wa Namungo, Hassani Zidadu, alisema kuwa "Tumefarijika kwa udhamini huu ambao SportPesa imetupatia ambao kwetu ni mkubwa.


"Udhamini huu utatuwezesha kununua tiketi za ndege na matumizi mengine kuelekea Sudan kwenda kucheza mchezo wetu dhidi ya Hilal.

"Kama unavyofahamu mchezo wa mpira wa miguu unahitaji fedha nyingi, hivyo kwa udhamini huu tunaamini kuwa utatusaidia kwa kiasi kikubwa katika kuelekea mchezo huo ambao ni mgumu, tunahitaji kupata ushindi ili tusonge mbele," alisema Tarimba.

"Ningependa kutoa rai kwa kampuni binafsi na za michezo kujihusisha ili kusaidia timu mbalimbali za mpira wa miguu kwani michezo ni sehemu ya burudani na ndio maana mpira wa miguu ni mchezo wenye mashabiki wengi zaidi."

# Michezo

Jumapili Januari 3, 2021
Nipashe



Solskjaer: Mbio za ubingwa EPL ngumu UKURASA 22



Mshambuliaji wa Manchester United, Anthony Martial (kushoto), akifunga bao huku golikipa wa Aston Villa, Emiliano Martinez, akishindwa kuokoa hatari hiyo langoni mwake katika mechi ya Ligi Kuu England iliyochezwa kwenye Uwanja wa Old Trafford juzi usiku. United ilishinda mabao 2-1. **PICHA: MTANDAO**

# SIMBA YAANDAA RAMANI YA 'VITA'

## ●●● Yaweka wazi FC Platinum ilitangulia lakini wao wamejipanga kumaliza...

**Na Saada Akida**

UONGOZI wa Simba umewaondoa hofu mashabiki wa klabu hiyo kuelekea mechi ya marudiano ya mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya FC Platinum kutoka Zimbabwe, itakayochezwa Jumatano kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam.

**Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Ofisa Mtendaji Mkuu wa Simba, Barbara Gonzalez alisema kwa upande wa uongozi wamejipanga vizuri na wameweka mikakati ya kuhakikisha wanapata ushindi na kusonga mbele katika mashindano hayo.**

Gonzalez alisema kikosi chao kimejiimarisha na kuufanyia kazi upungufu uliotokea katika mechi ya kwanza ili 'kuwamaliza' wapinzani wao hapa nyumbani.

Kiongozi huyo alisema kila idara katika kikosi chao imeimarika na matokeo ya mechi mbili zilizopita (Majimaji na Ihefu FC), yamewaongezea nguvu ya kuwakabili FC Platinum.

"Viongozi tumeweka mikakati yetu kwa ajili ya mechi hiyo ya marudiano na kikosi kipo imara, ukiangalia mechi mbili za mwisho tumepiga 5G (5-0) na 4G (4-0), kwa ushindi huu tunastahili kuendelea hivi katika mechi yetu ijayo ya Ligi ya Mabingwa Afrika, tumejipanga, hawatoki kwa Mkapa," alisema Gonzalez.

Aliongeza wana imani ya kufanya vyema katika mechi hiyo kutokana na mipango ya benchi lao la ufundi linaloongozwa na Sven Vandenbroeck ilivyoandaliwa.

"Ni mechi itakayokuwa na ushindani mkubwa, tumedhamiria kuhakikisha wachezaji wetu wanapambana kutafuta matokeo mazuri na kufuzu katika hatua nyingine," alisema kiongozi huyo.

Naye golikipa chaguo la kwanza la timu hiyo, Aishi Manula, aliliambia gazeti hili kikosi chao kina nafasi kubwa ya kupata ushindi na kwenda hatua inayofuata kutokana na kuwafahamu vyema wapinzani wao.

"Tumekuwa na rekodi nzuri tunapokuwa uwanja wa nyumbani, wametangulia lakini sisi tutawahi kufika, tunaamini mambo yatakwenda vizuri na kila shabiki wa Simba atafurahi," alisema Manula.

Golikipa huyo alisema tofauti ya bao 1-0 waliyonayo mpaka sasa haiwaumizi kichwa kwa sababu wanajua zimebaki dakika nyingine 90 za kupambana.

"Matokeo mazuri tuliyopata katika mechi zetu mbili tulizocheza hapa nyumbani yametuongezea morali kuelekea mchezo huo wa kimataifa, tunaamini nafasi ya kufuzu kwenda hatua ya makundi ni yetu," Manula alisema. Simba inahitaji ushindi wa kuanzia mabao 2-0 ili isonge mbele katika mashindano hayo na endapo itatolewa, itaangukia kwenye mchezo wa mtoano wa michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika.

Wakati huo huo, FC Platinum ilitarajiwa kuwasili nchini jana, tayari kwa mchezo huo wa marudiano utakaochezwa kuanzia saa 1:00 usiku.

## Carlinhos ndani Mapinduzi Cup

**Na Saada Akida**

BAADA ya kutoonekana kwa muda mrefu uwanjani, kiungo wa Yanga, Carlos Sterio 'Carlinhos', atakuwa katika msafara wa timu hiyo utakaoelekea Visiwani Zanzibar kwa ajili ya kushiriki mashindano ya Kombe la Mapinduzi, imeelezwa.

Meneja wa Yanga, Hafidh Saleh, aliliambia gazeti hili jana kuwa baada ya mapumziko ya siku mbili, kikosi cha timu yao kinatarajia kuingia kambini leo ili kujiandaa na mashindano hayo yaliyopangwa kufanyika kuanzia keshokutwa.

Saleh alisema afya ya Carlinhos imeimarika na yuko tayari kurejea uwanjani kuitumikia timu yake.

"Alikuwa anaendelea na mazoezi mepesi kama alivyoelekezwa na daktari, ila sasa anarejea kwenye kikosi na atakuwa miongoni mwa wachezaji watakaokwenda Zanzibar, mchango wake ni muhimu sana katika kufikia malengo," alisema meneja huyo.

Alieleza wachezaji wote wa Yanga watakuwa kwenye safari hiyo, isipokuwa nyota wake walioitwa kwenye kikosi cha Timu ya Taifa (Taifa Stars), ambacho kinajiandaa kucheza mechi ya kirafiki ya kimataifa dhidi ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC).

"Hakuna majeruhi mpya, kuhusu Carlinhos atakuwa miongoni kwa wachezaji watakaokwenda Zanzibar kwa sababu ameshapona na ameanza mazoezi mepesi, suala la kucheza katika michuano hiyo litabaki katika mipango ya Kocha Mkuu, Cedric Kaze," alisema Saleh.

Aliongeza kikosi chao kipo vizuri na kinaamini mwaka huu kitachukua kombe la michuano hiyo baada ya kulikosa kwa muda mrefu.

Nyota wa Yanga ambao wameitwa katika kikosi cha Taifa Stars kilichoko chini ya Mrundi Etienne Ndayiragije ni pamoja na Yassin Mustapha, Bakari Mwamnyeto, Feisal Salum 'Fei Toto', Ditram Nchimbi, Deus Kaseke na Farid Mussa.

Yanga itaanza kampeni ya kuwania kombe hilo kwa kuvaana na Jamhuri Januari 5, kwenye Uwanja wa Amaan wakati siku inayofuata watani Simba watawakabili Chipukizi.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042
9 770856 541002 >